epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Ijumaa Aprili 5, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581637

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**REAL KUACHANA NA KEPA**



# Samia: Watu wanadai katiba yao

- **Ataja** sababu uteuzi wa Makonda na wenzake; aagiza hoja zote za CAG zijibiwe... *Endelea ukurasa 2*

**LHRC** yabaini kasoro sheria mpya uchaguzi



UKURASA 4

**BoT** yaongeza riba kwa benki, thamani ya Shilingi yashuka



UKURASA 3

**Biteko** atangaza kibano watendaji wa TANESCO



UKURASA 8

## Mikopo elimu ya juu mtihani, wanafunzi 'wakacha' masomo

UKURASA 4



"Hakuna Waziri ambaye hakufundishwa na walimu, wala hakuna mbunge ambaye hakufundishwa na mwalimu. Malalamiko ni makubwa zaidi kwa kundi hili.

**JANEJELLY JAMES**



"Turudi tukae tuwasikilize watumishi kwani hiyo fedha ni yao, serikali inaweka. Wapeni mafao kwa mkupuo wa asilimia 50, hizo zingine muwape kidogokidogo.

**ESTER BULAYA**



"Wakija kustaafu licha ya uzoefu wao wote, eti wakishazeeka tunaona hawawezi kutunza fedha zao wenyewe. Hili si jambo jema.

**KASALALI MAGENI**

# Kikokotoo cha mafao moto bungeni

UK.3

**MICHEZO** **SIKU YA HUKUMU SIMBA, YANGA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Samia: Watu wanadai katiba yao

Na Romana Mallya



Aliyekuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Christian Makonda, akila kiapo mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani), kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. PICHA: IKULU

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema watu wanadai katiba yao, akielekeza Wizara ya Katiba na Sheria kufanyia kazi suala hilo.

Mkuu wa Nchi alitoa kauli hiyo jana Ikulu, jijini Dar es Salaam katika hotuba yake baada ya kuapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni.

Akitoa maelekezo mahsusi kwa Naibu Waziri mpya wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini, Rais Samia alisema, "Wewe (Sagini) ni mzoefu serikalini. Nenda kasaidie katika katiba na sheria. Kipindi hiki tulichonacho watu wanadai katiba yao, nenda kasaidiane na waziri, ninaimani utafanya vizuri."

Baada ya kuwapo mvutano wa muda mrefu katika serikali, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na vyama vya upinzani, hatimaye Juni 2022, chama tawala kilitangaza kuridhia kufufua mchakato wa Katiba Mpya uliokwama tangu mwaka 2015, yaani miaka 10 iliyopita.

Mnamo Juni 22, 2022, aliyekuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alitangaza chama hicho kimekubali kufufua mchakato wa Katiba Mpya, wakiwa na angalizo kwamba uzingatie maslahi ya taifa.

"CCM tunasisitiza umuhimu wa kuwapo Katiba Mpya kwa kuzingatia mazingira ya sasa na kuona namna bora ya kufufua, kukwamua na kukamilisha mchakato wa Katiba Mpya kwa maslahi mapana ya taifa na maendeleo kwa ujumla," alisema Shaka ambaye sasa ni Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro.

Wakati wa mkutano wa mwaka jana wa Bunge la Bajeti, serikali ilitangaza kuongeza takriban Sh. bilioni tisa katika bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2023/24, ili kukwamua mchakato wa Katiba mpya uliokwama Aprili 2, 2015, kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutangaza kuahirisha kura ya maoni ya Katiba Inayopendekezwa iliyokuwa ifanyike Aprili 30, mwaka huo.

Katika hotuba yake jana, Rais Samia alitoa maagizo kwa viongozi wateule, akichambua kila mmoja, kibarua kilichoko mbele yake na matokeo anayotaka.

Rais pia aliagiza hoja zote za ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alizokabidhiwa Machi 28, mwaka huu, zifanyiwe kazi mara moja ili Bunge linapozijadili ripoti hizo, hoja ziwe zimeshajibiwa.

Alitaja sababu za mabadiliko hayo aliyoyaita ya kawaida ni kuimarisha ufanisi katika kutoa huduma kwa wananchi.

Rais Samia alielekeza viongozi hao wakafanye kazi ya kuunganisha watu na kutatua migogoro iliyoko katika maeneo walikoteuliwa na si kwenda kuitengeneza.

**WENYE MIGOGORO**

Akitoa maelekezo kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulevamu), Degratius Ndejembi, Rais Samia alimweleza kuwa wameamua kumpandisha kutoka Naibu waziri kuwa Waziri kamili kutokana aliyofanya maeneo mbalimbali.

"Umesaidia vizuri mawaziri uliofanya nao kazi na tumeona na wewe ukashike hapo. Na ni matumaini yangu utakwenda kufanya vizuri. Ninadhani utakwenda kufanya yote, mbali ya kusimamia taasisi mbalimbali, una watu wenye ulemavu na vijana.

"Na vijana ndio wanafanya nusu (ya watu) ndani ya nchi, wanatarajia makubwa kutoka kwako. Wizara inasimamia sera na mipango ya makundi haya, kazi yako nenda karatibu sekta zote zinazohusika na vijana," aliagiza.

Rais alisema kazi kubwa ya waziri huyo mpya ni kuhakikisha vijana wanapata mafunzo na kupata maeneo ya kufanya kazi, ajira na kujiajiri.

Alionya viongozi wa wizara hiyo kuwa hataki kusikia wanagongana kwa kuwa ni vijana na watendaji watakaokuwa na migogoro wataondoka wote.

**RIPOTI ZA CAG**

Rais Samia pia alimtaka Waziri Ndejembi na mawaziri wengine kushughulikia yale yote yaliyoainishwa ndani ya Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2022/23, yasimamiwe na kufanyiwa kazi na hoja zijibiwe mara moja ili Bunge litakapozijadili, ziwe zimejibiwa tayari.

"Na mkijibu kwa haraka tutajua yapi yamejibiwa na yapi bado na hatua gani zichukuliwe. Wote mkasimamie hayo," Rais Samia aliagiza.

Kuhusu uteuzi wa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Zaibabu Katimba, Rais alisema kuwa pamoja na 'upya wake serikalini', ni mbunge mzuri mwenye uzoefu ndani ya Bunge na anayejua yanayoulizwa kwa serikali, hivyo akafanye kazi.

"Nimekuweka TAMISEMI, wizara pana yenye mambo mengi na wewe ni mdogo, ninajua utakwenda haraka na waziri wako (Mohamed Mchengerwa) ni mzuri sana. Timu ya TAMISEMI sasa hivi ni nzuri sana, nenda kashirikiane mfanye kazi. Suala kubwa ni asilimia 10 kwa vijana, Ndejembi atakuja kukaa kooni," alisema.

**TRAFIKI BARABARANI**

Akitoa maelekezo kwa Naibu Waziri mpya wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Daniel Sillo, Rais Samia alimweleza kuwa yale aliyokuwa akiwaambia akiwa mwenyekiti wa kamati ya Bunge anakwenda kuyaona katika wizara hiyo.

"Fedha inayoingizwa itoshe na mambo yaende. Upo field (eneo la kazi) sasa haupo katika kiti cha theory (nadharia). Kamsaidie waziri, wizara hii ina mambo mengi mno na sasa tunaibadili, tunataka iende kieletroniki.

"Tunataka vituo vyako vya polisi vilivyoko Rorya vitoe taarifa siku hiyohiyo matukio yakitokea na Mkuu wa Jeshi apokee ripoti.

"Usalama barabarani tunataka kuondoa trafiki, tunataka kuondoa rushwa, tuweke kamera na mambo mengine, ambayo yatafanya kazi automatically (moja kwa moja) kusiwe na (askari wa) usalama barabarani.

"Pia weee nenda, wee subiri, wee ahaa...! Kuna mambo mengi miradi mikubwa inasubiri ukifika huko waziri atakuongoza," alisema.

**JAMII NAMBA**

Rais Samia, akizungumzia uteuzi wa Maryprisca Mahundi, alisema, "Nimefanya makusudi kumbadilisha, ni mwanasheria, ambaye sasa ni Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, anakwenda kumsaidia Waziri Nape (Nnauye).

"Kuna mambo mazuri jana (juzi) umeona (uzinduzi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi), nenda kasimamie, kuna mikataba mikubwa wanaingia, kasaidie kuweka jicho la kisheria.

"Nilitoa agizo Watanzania wote kila mtu awe na namba yake, wenyewe wameipa jina 'Jamii Namba', nenda kasimamie hii tujuane humu ndani nani ni nani, haiwezekani mtu mmoja ana identities (vitambulisho) tatu".

**UBAMBIKIAJI BILI**

Kwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Kundo Mathew, Rais alimtaka kuhakikisha maji yanafika kwa wananchi kwa kuwa CCM imewataka ifikapo mwakani, wawe wameyasambaza kwa asilimia 95 mijini na asilimia 85 vijijini ambapo wanaamini watazidi asilimia hizo.

"Nenda mkasimamie vijijini ifike asilimia 87 tuliyojiwekea, isipofika mniambie wapi mmezubaa. Kuna miradi lazima imalizike.

"Bili za maji ni kilio cha wananchi, tumelia sana na kubambikwa bili za maji, mkaenda kwenye mita, bado kuna kilio, fanyeni kama TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania). Tafuteni mita ambazo watalipa namna wanavyotumia.

"Nimesikia mmewahi kuziagiza na zimepimwa zina matatizo madogo karekebisheni mzifunge kwa wananchi na zitawafundisha matumizi ya maji," alisema.

**MOTO WA MAKONDA**

Rais Samia alipongeza utendaji wa Paul Makonda katika siku 162 akiwa Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, akibainisha kuwa amefanya kazi kubwa ndani ya chama kwa kukichemsha kwa kutoa uvivu uliokuwa kwa kila mmoja.

"Umekichemsha chama. Tumeamka vizuri sana. Tumekupeleka Arusha, unajua nini kipo Arusha. Unajua matumaini yangu Arusha. Mimi nina matumaini nawe. Utafanya kile ambacho mimi ninatamani ukafanye," Rais alielekeza.

Rais Samia alimweleza Mkuu huyo mpya wa Mkoa wa Arusha kwamba utalii jijini Arusha umekua, wageni ni wengi, malazi hayatoshi, hivyo kumtaka akasimamie suala hilo kwa kushirikiana na wawekezaji.

"Arusha ni mji mkubwa sana na ni Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na taasisi kubwa za kiulimwengu zipo pale. Nenda kasimamie vizuri mkoa uwe na jina zuri," aliagiza.

Kuhusu Mkuu mpya wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi, Rais alisema mkoa huo kutokana na wasifu wake, ameona huyo ndiye anaweza kufanya yote ikiwamo kuinua mikoa ya Mara na Kagera kwa kushirikiana na mwenzake walioko ukanda hao.

Alisema kuna kilimo mkoani Mara ambacho hawakipendi, lakini ni kizuri kwa biashara, hivyo akakisimamie kwa sheria, kwa kuwa kuna watu wa serikali wanakisindikiza kwa magari yao baada ya kuvunwa kwenda nchi jirani.

Pia alimtaka akasimamie mpaka na hifadhi zilizoko huko, pia kukuza utalii.

Kuhusu Naibu Katibu Mkuu, Rais Samia aliwataka wakafanye kazi vizuri, huku akimtaja Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Suleiman Serera, kuwa ni kijana mdogo na ataweka jicho la karibu kwake kwa kumfuatilia na kumshauri ili akue vizuri.

**MAHAKAMANI**

Rais Samia pia alitaka Sylvester Kainda, Jaji Mahakama Kuu ya Tanzania, akasimamie haki kwa wale wanaostahili kuzipata na wasio na haki asiwape.

Katika hafla hiyo, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema, "Suala la mazingira linamgusa kila mmoja, niwaombe sana mazingira ya nchi yameharibika, tuna wajibu wa kuyarejesha ili nchi iendelee kustawi."

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema Rais ana imani na viongozi hao alioteua hivi karibuni, hivyo wafike kwa wananchi kusikiliza na kuwapa huduma kwa kutatua kero zao na kutimiza malengo.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema, "Bahati nzuri mmepata imani hii katika kipindi ambacho Bunge la Bajeti linaendelea, hivyo hakutakuwa na muda mrefu wa kujifunza kwa ninyi tunaowatarajia kuja bungeni kujibu hoja za wabunge."

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alisema watendaji wa mahakama walioapishwa wataongeza nguvu ya kutenda haki mahakamani.

"Wale wanaopeleka changamoto zao za kisheria kwako Mheshimwa Rais, ninaomba wawe wanapeleka kwa Msajili wa Mahakama, ndiye anayeshikilia injini ya mahakama na ndiye anajua inakoelekea," alisema.

Uteuzi wa wakuu wa mikoa na mawaziri ulitangazwa usiku wa kuamkia Jumapili ya Pasaka, uteuzi wa Prof. Joyce Ndalichako katika nafasi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri ukitenguliwa.

**HABARI KITAIFA**



Ofisa ugani wa Kata ya Mihumo, wilayani Liwale mkoani Lindi, Rashid Makubui, akitengeneza njia mbadala ya kufukuza tembo shambani kwa kutumia mchanganyiko wa pilipili, tangawizi, majani ya mwarobaini na mafuta ya kula. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kikokotoo cha mafao moto bungeni

**Na Vitus Audax,** DODOMA

SAKATA la kikokotoo cha mafao kwa wastaafu, limeibuka tena bungeni huku Mbunge wa Viti Maalum, Ester Bulaya, akisema bado ni janga.

Kutokana na hali hiyo, ameiomba serikali kukaa meza moja na wadau ili kujadili namna bora ya kuwapa mafao yao kutoka asilimia 33 iliyopo sasa hadi 50 kwa mafao ya mkupuo.

Akichangia jana Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa mwaka 2023/2024 na Mwelekeo wa Kazi zake kwa mwaka 2024/25 bungeni, jijini hapa, Bulaya alisema: "Sote tunajua kikokotoo bado ni janga na hii haijaisha mpaka iishe kwani bado kuna manung'uniko kwa watumishi. Nikiwaonyesha meseji zangu kutoka kwa walimu, maaskari, madaktari na wengine ni shida. Mtu anastaafu anapewa Sh. milioni 17 hajajenga.

"Inajulikana kuwa watumishi hao wanafanya kazi kwenye mazingira yapi, hivyo kuteleza siyo kuanguka. Turudi tukae tuwasikilize kwani hiyo fedha ni yao, serikali inaweka. Wapeni mafao kwa mkupuo wa asilimia 50, hizo zingine muwape kidogo kidogo."

Alisema fedha za mafao ya mkupuo ndizo zinazowasaidia wala si hizo za kila mwezi kwa kuwa wakishaweka misingi kupitia fedha hizo, mambo mengine yatakwenda kama kawaida. Alisema madhara hayo yanasabashwa na kupitishwa kwa sheria hiyo kwa lazima.

"Leo mifuko yetu ina shida lakini mimi nazungumzia mfuko mmoja tu hapa wa wawatumishi wa serikali (PSSSF) kwani Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii inatakiwa iwe japo asilimia 40.

Kwa nini ripoti ya CAG (Mdhibniti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) ionyeshe kila mwaka uko asilimia 20?," alihoji.

Alidai kuwa serikali inachukua fedha kwenye mfuko na kuenda kuwekeza lakini hailipi, akitolea mfano wa mwaka 2020/21 alisema serikali ililipa kwa 'non cash bond' zaidi ya Sh. trilioni 2.1 na kuahidi kuwa mwaka unaofuata ingelipa Sh. trilioni 2.4 ambayo hadi sasa haijalipwa.

"Sasa hii mifuko itawezaje kuwa 'stable' (imara)? Nikianza kwa takwimu za Juni, 2020 tunaona michango ya wanachama kwenye mfuko ilikuwa Sh. bilioni 1.364 na mahitaji ya mafao yalikuwa Sh. bilioni 1.554. nyongeza waliyochukua kwenye vyanzo vingine ilikuwa Sh. milioni 190," alisema.

Pia alisema kwa mwaka jana, michango ya wanachama kwenye mfuko ilikuwa Sh. bilioni 1.526 wakati mahitaji ya mafao yalikuwa Sh. bilioni 1.567 nyongeza waliyochukua kwenye vyanzo vingine ilikuwa Sh. milioni 171.

Kwa mwaka huo, alisema uwekezaji ulikuwa Sh. milioni 587 na kwamba mfuko huo kuwa ndio unaotegemewa na watumishi Pamoja na serikali ambayo inakopa kuwekeza katika maeneo mbalimbali lakini inapata hasara katika uwekezaji husika.

Mbunge wa Sumve (CCM), Kasalali Mageni, alisema suala la kikokotoo lina hoja kutokana na madai kuwa watumishi wa serikali wana uwezo mdogo wa matumizi na utunzaji fedha, hivyo wakipewa fedha hawatazitumia vizuri, hivyo serikali iwatunzie na kuwapatia kidogo kidogo.

"Naomba tujadiliane suala hili kwa kuwa hawa watumishi ndio leo wako kwenye ofisi, wametuletea makabrasha yote tunayojadili bajeti hii na wamepanga kila kitu. Wanalinda na kufanya shughuli zote muhimu nchini. Lakini wakija kustaafu licha ya uzoefu wao wote, eti wakishazeeka tunaona hawawezi kutunza fedha zao wenyewe. Hili si jambo jema," alisisitiza

Alisema licha ya serikali kuliona jambo hilo ni zuri, mitaani bado halijawaingia wahusika akilini na hawalielewi huku wale ambao wamelazimika kuingia kwenye kikokotoo, wengi wao limewachanganya wengine hadi kufariki dunia kwa mawazo.

Naye Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Janejelly James, aliiomba serikali kuongeza kasi ya kulipa maslahi ya wastaafu hususani walimu. Alisema katika kada hiyo kuna kilio kikubwa licha ya kutegemgewa zaidi katika kulijenga taifa kielimu.

"Hakuna Waziri ambaye hakufundishwa na walimu wala hakuna mbunge ambaye hakufundishwa na mwalimu. Malalamiko ni makubwa zaidi hata leo Waziri Jenesta (Mhagama- Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge) nikikuletea ujumbe niliopokea hapa uone wanavyolalamika zaidi,"alisema.

Alisisitiza pia juu ya umuhimu wa watumishi kufikishiwa elimu ya kikokotoo ipasavyo kwa kuwaambia faida na hasara zake kwa kuwa bado wako kwenye giza hawaelewi kile wanacholipwa ni nini na kwa nini.

## BoT yaongeza riba kwa benki, thamani Shilingi yaporomoka

**Na Maulid Mmbaga**

KAMATI ya Sera ya Fedha (MPC) imepandisha kiwango cha riba ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutoka asilimia 5.5 hadi sita, ambayo itatumiwa na benki nchini katika robo ya pili ya mwaka huu kuanzia Aprili hadi Juni, huku ikibainisha kushuka thamani ya shilingi dhidi ya dola kutoka asilimia 1.6 mwaka 2023 hadi 1.8.

Uamuzi wa kupandisha riba ya BoT ulifikiwa katika kikao cha kamati hiyo kilichofanyika juzi, ambacho kilizingatia tathmini ya mwelekeo wa uchumi iliyofanyika Machi, mwaka huu.

Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa kamati hiyo imeona umuhimu kuongeza riba itakayokuwa na wigo wa asilimia mbili ili kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei siku zijazo kutokana na athari za mwenendo wa uchumi wa dunia.

"Kamati imeridhishwa na kuendelea kuimarika kwa uchumi nchini licha ya changamoto zilizotokana na mtikisiko katika uchumi wa dunia. Tuna akiba ya kutosha ya fedha za kigeni dola bilioni 5.3 ambayo itawezesha huduma na kuagiza bidhaa mbalimbali kutoka nje kwa miezi minne.

"Thamani ya Shilingi dhidi ya dola pia ilipungua kwa asilimia 1.8 katika robo ya kwanza ya mwaka huu ikilinganishwa na asilimia 1.6 katika robo ya mwisho ya 2023. Hali hii ilitokana na msimu wa mapato madogo ya fedha za kigeni pamoja na mazingira ya kiuchumi duniani," alisema Tutuba.

Aidha, alisema kamati hiyo pia ilijadili kuhusu upungufu wa fedha za kigeni nchini na kujiridhisha kwamba hatua za kuongeza upatikanaji na kupunguza matumizi ya dola zinazotekelezwa sasa zinatarajiwa kupunguza changamoto hiyo ndani ya muda mfupi ujao.

Mwenyekiti wa Umoja wa Benki Tanzania (TBA), Theobald Sabi, alisema riba hiyo ni lazima kuiangalia kwa muktadha wa kiuchumi, akieleza kuwa viwango vya mikopo chechefu vimeendelea kushuka hadi asilimia 4.5 katika soko zima la kibenki.


OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI
(IDA CREDIT NO. 7215-TZ)

**TANGAZO KWA UMMA**

**ZOEZI LA UBOMOAJI WA NYUMBA ZILIZOFIDIWA NA MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**

Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) alianza kuwalipa fidia waathirika wa mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kuanzia mwezi Novemba 2023. Kwa mujibu wa makubaliano ya ulipaji wa fidia, waathirika wanatakiwa kupisha eneo la mradi ndani ya wiki sita (6) baada kupokea fedha kwenye akaunti zao. Muda huu umeshakamilika kwa idadi kubwa ya waathirika.

Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa kushirikiana na ofisi za Wakurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Kinondoni, inatarajia kuendesha zoezi la ubomoaji wa nyumba zilizofidiwa kuanzia tarehe 12/04/2024. Hivyo waathirika wa mradi wanatakiwa kupisha eneo la mradi kabla ya tarehe tajwa hapo juu. Ikumbukwe kuwa ubomoaji huu unawahusu waathirika wa mradi ambao wameshapokea fidia katika akaunti zao kwa muda usiopungua wiki sita (6) tangu siku ya kuanza zoezi hili.

KATIBU MKUU
OFISI YA RAIS - TAMISEMI



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Alhikma Foundation, Nurden Kishki (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu taasisi hiyo kugharamia safari ya waislamu 10 kwenda hijja kupitia Jukwaa la Hijja. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mikopo elimu ya juu mtihani

## - Serikali yabanwa wanafunzi kukatisha masomo vyuoni

**Na Vitus Audax,** DODOMA

UTOAJI mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini umeibua hoja bungeni.

Mbunge wa Ngara, mkoani Kagera, Ndaisaba Ruhoro ametaka serikali kuingia mitaani kufanya uchunguzi ili kubaini idadi kubwa ya vijana walioacha kuendelea na masomo yao ya vyuo vikuu na kurudi mitaani kutokana na wazazi wao kushindwa kugharamia masomo yao.

Amesema wakishawapata vijana hao, wapelekwe Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ili wapatiwe mikopo na kuendelea na masomo yao ili kutimiza ndoto zao na kukomboa wazazi wao.

Ruhoro aliyasema hayo bungeni jijini hapa jana wakati akichangia hoja ya Waziri Mkuu kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema kuwa licha ya mpango wa serikali kutoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, wapo ambao wamekuwa wanakosa licha ya kuwa na vigezo vya kupata ufadhili huo.

Alisema dhamira ya HESLB ni kuhakikisha wanafunzi wanawezeshwa kusoma elimu ya vyuo vikuu na vyuo vya kati.

“Kwa sasa hali imekuwa mbaya zaidi kama ilivyo katika ngazi za chini - idadi kubwa ya wanafunzi kuacha masomo yao - hali hiyo imegeukia katika upande wa vyuo vikuu wanafunzi wengi wanaacha masomo yao. “Hivi tunavyozungumza, wabunge tunabanwa huku kusaidia watoto walioshindwa kuendelea na vyuo vikuu. Ukiuliza unaambiwa mzazi amekosa mkopo na wazazi wameuza mifugo, mazao, viwanja wengine hadi wanauza nyumba zao ili wapate fedha ya kuwasomesha, lakini bado hali inashindikana njiani, wanashindwa kuhimili miaka hiyo mitatu,” alisema Ruhoro

Alisema hali hiyo inasababisha wananchi kuuza mali zao bila mafanikio na kukosa yote na kueleza kuwa hadi juzi alikuwa amepokea vijana sita wanaohitaji ufadhili kwake kuendelea na masomo yao kutokana na kukosa mikopo.

Alitaka serikali iende vyuoni na kufuatilia wote walioandika barua kuacha masomo vyuoni warudishwe kwa ufadhili wa HESLB kama lilivyo lengo la serikali kupitia bodi hiyo.

Januari 4, mwaka huu, Nipashe, baada ya kuzungumza na wanafunzi waliolalamika kunyimwa au kupatiwa mkopo ‘kiduchu’, iliwasiliana na Mkuu wa Mawasiliano wa HESLB, Omega Ngole, aliyebainisha kuwa kwa mwaka huu wa masomo, hakuna mwanafunzi aliyepatiwa mkopo kwa asilimia 100 isipokuwa wenye ulemavu na waliopoteza wazazi wote wawili.

Katika hotuba yake bungeni juzi, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema serikali imeongeza fedha za mikopo ya elimu ya juu kutoka Sh. bilioni 654 kwa mwaka 2022/23 hadi Sh. bilioni 738.7 mwaka 2023/24.

Alisema wanufaika wa mikopo na ruzuku wameongezeka kutoka wanafunzi 177,615 mwaka 2022/23 hadi wanafunzi 220,278 mwaka 2023/24.

“Vilevile, serikali imeendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi wenye ufaulu uliojipambanua kupitia Samia Scholarship ambapo jumla ya Sh. bilioni 9.74 zilitolewa kwa wanafunzi 1,276 wanaoendelea na masomo katika fani za teknolojia, uhandisi, hisabati na tiba,” alisema.

**NYANZA MINES (T) LTD
DRILLING OF BOREWELLS IN
UVINZA, KIGOMA**

**QUOTATIONS ARE INVITED TO:**
1. **DRILL 2 BOREWELLS**
2. **REHABILITATE 3 BOREWELLS**

DEPTH OF THE BOREWELLS – 200 MTRS
DIAMETER OF UPVC CASING - 315 MM

THE QUOTATION WILL INCLUDE PUMP TESTING FOR 48 HOURS FOR DELIVERY OF 100 CU MTRS PER HOUR, DETERMINATION OF DRAWDOWN LEVEL AND ALL OTHER REQUISITE TESTING

**FOR FURTHER DETAILS CONTACT:
OPEARTIONS MANAGER, Tel 022-2123640
Email: nsalt@nyanzamines.co.tz**

# LHRC yaona kasoro sheria mpya uchaguzi

**Na Enock Charles**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimekosoa watumishi wa umma kuendelea kuwa sehemu ya Tume ya Uchaguzi katika sheria mpya iliyotiwa saini na Rais Samia Suluhu hivi karibuni, hivyo kutaka tume kuajiri watumishi wake ili kuipa uhuru wa kutosha.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, alisema hayo jana baada ya kufanya uchambuzi wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 2 ya mwaka 2024, Sheria ya Vyama vya Siasa 2024, na Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya mwaka 2024.

Alisema kitendo cha watumishi wa umma kuendelea kuwa watumishi wa Tume ya Uchaguzi kinapunguza uaminifu na uhuru wa tume hiyo.

“Miongoni mwa mambo ambayo LHRC na wadau wengi tulishauri ni tume kuajiri watumishi wake yenyewe ili kuipa uhuru wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake na kuongeza uaminifu kwa wadau wa uchaguzi. Pendekezo hili halikuchukuliwa badala yake watumishi wa umma wameendelea kuwa sehemu ya tume.

“Kifungu cha sita cha sheria hii kimeondoa neno wakurugenzi wa halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji na kuweka neno watumishi wa umma waandamizi kuwa wasimamizi wa uchaguzi. Kifungu cha saba cha sheria kimeendelea kuwatambua wakurugenzi wa halmashauri kuwa maofisa uandikishaji wapigakura,” alisema.

Pia alisema kifungu cha nane kimeendelea kuwatambua watumishi wa umma kuwa waratibu wa uchaguzi katika ngazi za mikoa, hivyo kwa tafsiri ya kisheria ni kwamba wakurugenzi wa halmashauri kwa nafasi zao bado wanaweza kuwa wasimamizi wa uchaguzi suala ambalo linaendelea kutotibu wala kuleta afueni ya mifumo ya uchaguzi ambayo imekuwa ikilalamikiwa kwa muda mrefu.

Pia alizingumzia kuhusu watendaji wa tume wakiwamo mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe waliopo sasa kuendelea kutumikia nafasi zao hata baada ya kuanza kutumika kwa sheria mpya mpaka pale watakapomaliza utumishi wao baada ya miaka mitano.

“Licha ya wadau wengi kufurahishwa na kuchukuliwa kwa pendekezo la muda mrefu la kuwepo kwa mfumo huru wa namna ya kupatikana kwa tume na licha ya kifungu cha 10 cha sheria kuanzisha kamati ya usaili kwa ajili ya kuwapata mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe wengine wa tume, kwa wakati huo huo kifungu cha 27 cha sheria kinasema mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe wa tume waliopo sasa wataendelea na nafasi zao hata baada ya sheria hii kuanza kutumika rasmi.

“Kwa lugha rahisi ni kwamba kamati ya usaili iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 9 cha sheria haitaanza kazi ya kusaili mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe wengine wa tume waliopo madarakani hivi sasa mpaka pale watakapomaliza nafasi zao za utumishi baada ya miaka mitano.

“Kwa lugha nyingine mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe wengine wa tume watakoma katika nafasi zao kati ya mwaka 2028 na 2029 hivyo kamati ya usaili itaanza zoezi la kusaili watu hao,” alisema.

Kuhusu suala la uamuzi wa tume kutokuhojiwa mahakamani licha ya jambo hilo kupigiwa kelele na wadau wengi, alisema kitendo hicho kinakiuka ibara ya 13(6)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

“Kwa mujibu wa vifungu vya 36(6),53 (6) na 65(7) vya sheria maamuzi ya tume juu ya mgombea urais, ubunge, na udiwani kukataliwa uteuzi yatakuwa ya mwisho na hayatahojiwa mahakamani kitendo ambacho wadau tulithibitisha kinakiuka Katiba,” alisema Dk. Henga.

Kuhusu suala la mgombea binafsi, alisema ulikuwapo uamuzi wa mahakama za ndani na za kikanda kuruhusu kuwapo kwa mgombea binafsi lakini pendekezo hilo pia halijazingatiwa katika sheria mpya. Ujumuishwaji wa masuala ya kijinsia, watu wenye ulemavu pamoja na vijana, alisema pia halijazingatiwa kikamilifu kama ilivyokuwa matarajio ya wadau ikiwamo kuviwajibisha vyama vya siasa ambavyo vitashindwa kuzingatia jinsia katika uchaguzi ndani ya chama na zile za kiserikali.

“Kwa mujibu wa kifungu cha 10C cha sheria, moja ya nyaraka za lazima ambazo chama cha siasa kitalazimika kuwa nazo ni pamoja na sera ya jinsia na ujumuishwaji. Hata hivyo, kifungu hiki hakijaweka mfumo wa kuviwajibisha vyama vya siasa ambavyo vitashindwa kutekeleza takwa hili,” alisema.



Wafanyakazi wa mkandarasi wakifanya maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi ya mwendokasi katika barabara ya Nyerere, eneo la Kamata, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# 72 mbaroni kuhusishwa dawa za kulevya

**Gwamaka Alipipi na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imesema imekamata kilo 54,506 za dawa za kulevya za mashambani na viwandani pamoja na kuwakamata watuhumiwa 72.

Pia, imekamata dawa mpya ya kulevya, Methylene dioxy pyrovalerone (MDVP) iliyo katika kundi la vichangamshi inayotengenezwa kwa kutumia kemikali bashirifu.

Wanaotumia huduma ya matibabu saidizi kwa waraibu wa dawa za kulevya, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), hadi Machi, mwaka huu ni 957 kati ya 3,794 ya waliosajiliwa kuanza tiba hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu wanaume wanaojihusisha na uraibu wanaongoza. Kati ya waliosajiliwa 3,794 wanaume ni 3,649 na wanawake ni 145.

Kamishna Jenerali wa DCEA, Aretas Lymo, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni waliyoifanya kwa kipindi cha Februari hadi Machi, mwaka huu, katika mikoa ya Shinyanga, Tabora, Iringa, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam.

Alisema katika operesheni hiyo wamekamata bangi kilo 54,489, mirungi (10.3), heroin gramu 90.93, cocaine gramu 1.98 na MDVP iliyokuwa ikisafirishwa na raia wa Comoro, Ahmed Abdou aliyekamatwa katika Jiji la Dar es Salaam.

Alisema dawa hiyo huuzwa kwa njia ya mtandao na husafirishwa kupitia kampuni za usafirishaji vifurushi na hufichwa kwa kuweka chapa za majina bandia.

Alisema DCEA imebaini kuwapo kwa mashamba makubwa ya bangi katika Hifadhi za Misitu ya Ubagu mkoani Shinyanga na mabatini, mkoani Tabora.

Alisema wahalifu hao wamekata miti katikati ya misitu hiyo na kulima bangi, kwa ushirikiano walioupata kutoka kwa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) waliteketeza mashamba hayo na kuwakamata wahusika

Wakati huo huo, kuhusu watumiaji Bingwa wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka MNH, Dk. Iddy Haruna, aliyasema hayo, aliwasilisha mada kuhusu huduma hiyo tangu ianzishwe, ilipofikia, changamoto na matarajio.

Mkutano huo, uliandaliwa na Wizara ya Afya, kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Mzumbe kwenye Uzinduzi wa Jumuiya ya Wadau wa Afya ya Akili (ECHO), kwa njia ya mtandao, jana.

Dk. Haruna, alisema miongoni mwa sababu zinazosababisha kuwapo idadi ndogo ya wanaopatiwa huduma hiyo, ikilinganishwa na waliosajiliwa, ni pamoja na wengine wamemaliza tiba, wamefariki, wamehama kituo ama wameacha matibabu.

Aidha bingwa huyo, alisema kuna mahitaji makubwa ya tiba hiyo, pamoja na wataalamu na kwamba hasi sasa idadi ya Vituo vya Tiba Saidizi kwa Kutumia Dawa (Medically Assisted Therapy-MAT), vimefikia 16, kikiwamo kilichopo Gereza la Segerea.

Alifafanua kwamba, kabla ya kliniki ya MAT, kuanzishwa nchini, kulikuwa ongezeko la Watu Wanaojidunga Dawa za Kulevya (PWID), takriban 50,000 huku wakichangia sindano na kushiriki ngono bila kondomu.

Alivitaja vituo vya MAT ambavyo ni 16 vilivyopo nchini ni MNH, Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mwananyamala, Hospitali ya Rufani ya Mkoa Temeke, Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, hospitali ya Sekou - toure, Mwanza; Hospitali ya Mirembe, Dodoma; Hospitali ya Bagamoyo, Pwani; Hospitali ya Bombo, Tanga.

Vituo vingine Hospitali ya Tumbi, Pwani; Hospitali ya Mount Meru, Arusha; Kituo cha Afya Tunduma, Songwe; Gereza la Segerea; Kituo cha Afya Tegeta, Dar es Salaam; Zahanati ya Mbagala na Hospitali ya Kigamboni.

# Ofisa Kilimo ashambuliwa, gari lake lachomwa moto

**Na Oscar Assenga,** MUHEZA

WAKAZI wa Kijiji cha Kambai, Kata ya Kwezitu, Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, wameamua kujichukulia sheria mkononi kwa kumshambulia kwa kipigo Ofisa Kilimo na kuliteketeza kwa moto gari lake baada ya kutopendezwa uamuzi wa kuwapa wawekezaji ekari 500 za ardhi bila kufanyika tathmini.

Kwa sasa, ofisa kilimo huyo, amelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Muheza.

Akizungumzia tukio hilo jana, Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainabu Abdallah, amekiri ofisa huyo kushambuliwa na gari lake alilokuwa akilitumia aina ya Suzuki, kuchomwa moto na wananchi waliokuwa wakimtuhumu kushindwa kusimamia maslahi yao na kusababisha wawekezaji kupewa eneo hilo.

"Ni kweli hilo tukio limetokea na baada ya kupokea taarifa hiyo, nililazimika kufika eneo la tukio kujionea uharibifu wa gari hilo na kufanya mkutano na wananchi ili kutafuta ufumbuzi wa suala hilo.

"Halmashauri (Muheza), ina eneo la zaidi ya ekari 3,000 lenye hati kwa zaidi ya miaka 28. Lakini ndani ya kipindi hicho cha miaka hiyo hawajaliendeleza.

"Na alipatikana mwekezaji wa kwanza mwaka 2020/2021 akapewa ekari 500 pasipo tathimini ya kina kufanyika. Mwaka jana, walipatikana wawekezaji wengine wanne, nao pia tathmini ya kina haikufanyika."


## SOUND AND FAIR TANZANIA KUPITIA WAFILISI WA PAMOJA KUTUPWA MALI, 2024

Kampuni ya Sound and Fair Tanzania Limited kupitia Wafilisi wa Pamoja inatarajia kutoa mali zake na hivyo inawaalika wazabuni kushiriki katika mchakato wa zabuni. Mali hizo zitauzwa kwa mnada wa wazi tarehe 9 Aprili 2024 kuanzia saa 9:00 asubuhi huko Mbagala-Kongowe, Mzinga. Wazabuni wenye nia wanahimizwa kutembelea yadi yetu iliyopo Mbagala- Kongowe, Mzinga kwa ukaguzi na uhakiki wa mali kwanzia tarehe 5 Aprili hadi 8 Aprili 2024.

**ORODHA YA MALI**

| S/N | JINA LA MALI | MAELEZO YA MALI | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1 | LAND | Land 16.51 acres, Nanjirinji Lindi | |
| 2 | SOLAR KILN | Solar Kiln, 7.5cm length 2016, Model:Type A Solar | 1 |
| 3 | TABLE SAW | Table Saw Nova Si 400 | 1 |
| 4 | DUST COLLECTOR | Woodworking CNC Router Dust Collector Wood Saw Dust Extractor, (Work Dust Control Co.) | 6 |
| 5 | SOLAR PANNEL | Solar Panel, 300W | 12 |
| 6 | SOLAR BETRY | Solar Battery, 2V/200Ah | 36 |
| 7 | FUEL TANK | Fuel Tank (Diesel Unit) capacity: 4500 liters | 1 |
| 8 | INVERTER CHARGER | Pure Sinewave Inverter Charger 1.6KW | 1 |
| 9 | CHAINSAW | CHAINSAW, Brand: Husqvarna, Model: 365 Special, Power Source: Petrol | 2 |
| 10 | TURNING MACHINE | Wood Turning Machine Lenze | 1 |
| 11 | SLINGSBY | SLINDSBY, Heavy Duty 2.5 tons Pallet Truck, for moving heavy staff maximum up to 2500kg | 1 |
| 12 | WATER PUMP | Submersible water pump 3 hp with motor three phase | 1 |
| 13 | CROSSCUT MASHINE | Dewalt Cross Cut Machine made in German | 1 |
| 14 | PRINTER | HP Laser jet Pro 176 N | 1 |
| 15 | TELEVISION | VON Hot Point type, Flat Screen, 42 inches | 1 |
| 16 | Mpingo | Unprocessed Mpingo logs | 493cm3 |

Mali nyingine ni pamoja na meza 3 za ofisi, rafu 3 za ofisi, kabati 4 za mafaili, viti 2 vya ofisi, vitanda 10, magodoro 10, kisimbuzi cha DSTV, printa 2, vizima moto 7, pampu ya maji na mtungi wa gesi.

Kwa habari zaidi, tafadhali wasiliana na:
Wafilisi wa Pamoja
Sound and Fair Limited
Barua pepe: straton@auditaxinternational.co.tz na khalfani@auditaxinternational.co.tz
Simu: +255 719 878 490

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jeshi la Polisi lijitafakari madai ya kumbambikia raia kesi ya ugaidi

**KWA** muda mrefu, Jeshi la Polisi limekuwa likilalamikiwa kwa kukiuka maadili na dhima ya majukumu yake ya kulinda usalama wa raia na mali zao, kwa baadhi ya askari na maofisa wake kujihusisha na vitendo vya rushwa, ubambikaji wa kesi dhidi ya wananchi zikiwamo za madai ya ugaidi.

Pia baadhi ya askari na maofisa wa jeshi hilo wamekuwa wakituhumiwa kushiriki katika vitendo vya ujambazi na kupora fedha za watu na hata kuwaua ili kupoteza ushahidi. Hata baadhi ya vidhibiti vya kesi vinavyoshiliwa katika vituo hivyo, vimekuwa vikidaiwa kuharibiwa na askari wasio waaminifu na matokeo yake kuipaka tope taasisi hiyo muhimu.

Kuwapo kwa malalamiko kutoka kwa wananchi, viongozi wakuu wa serikali mara kwa mara wamekuwa wakifanya mabadiliko ya wakuu wa jeshi hilo na kuwaagiza kutekeleza majukumu yao kwa weledi huku wakisisitiza kupambana na vitendo vinavyolichafua pamoja na kuwachukulia hatua wale wanaoshiriki vitendo hivyo.

Rais Samia Suluhu Hassan pia amekuwa akisisitiza mara kwa mara juu ya utendaji kazi wa Jeshi la Polisi kwa kuzingatia maadili na weledi. Sambamba na msisitizo wa Rais, Mkuu wa Jeshi hilo kwa sasa, Inspekta Jenerali (IGP) Camilus Wambura, amekuwa akifanya mabadiliko ya makamanda na wakuu wa vitengo kwa lengo la kuimarisha utendaji.

Katika mikutano kadhaa ya maofisa wakuu na waandamizi wa jeshi hilo, Rais Samia aliweka bayana kwamba jeshi hilo limepoteza imani kwa wananchi kutokana na baadhi ya maofisa na askari kujihusisha na vitendo vya aibu vikiwamo kubambikia kesi raia, kuomba na kupokea rushwa, kupora fedha na mali za raia, kutishia kuwabambikia kesi za ugaidi na vifo vya raia katika mahabusu zinazosababishwa na vipigo kutoka kwa polisi.

Kuwapo malalamiko hayo na vitendo vya dhahiri, Rais alimwagiza IGP Wambura kuhakikisha anawashughulikia wale wote wanaotuhumiwa kujihusisha na vitendo hivyo na kulirejesha jeshi katika ahadi yake na kuwafanya wananchi kuliamini.

Licha ya maagizo hayo, kumeibuka tena jambo zito la mwananchi kudai kuwa anahofia usalama wa maisha yake baada ya polisi kumtishia kumbambikia kesi ya ugaidi kutokana na kufuatilia mwenendo wa shauri lake katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Shinyanga kwa ajili ya kukata rufani.


Mwananchi huyo, Bertha Mabula, ambaye ni mfanyabiashara wa kusindika mazao, alifungua shauri lake katika mahakama hiyo dhidi ya Tumsime Tibaijuka ambaye alimkopesha Sh. milioni 295 lakini lilitupiliwa mbali. Lakini wakati anafuatilia hilo, ndipo kukawapo madai ya kundi la polisi waliokuwa wakimfuatilia ili kumkamata kwa madai ya ugaidi.

Imedaiwa kuwa polisi hao walimvizia eneo la Tinde kutaka kumkamata lakini walishindwa kutokana na mvua kubwa iliyonyesha lakini sasa kuna madai kwamba dereva aliyempeleka Shinyanga, alikamatwa kwa madai ya kumbeba gaidi na kufikishwa kituo cha polisi Kahama kisha kuhojiwa na kuachiwa.


Mazingira ya kukamatwa kwa dereva na mfanyabiashara kutuhumiwa ugaidi kwa kutaka kulipua jengo la mahakama kuu yanatia ukakasi na kuibua maswali yasiyo na majibu. Kuna uhusiano gani kati ya ugaidi na mtu anayefuatilia haki yake? Inakuwaje polisi wamvizie mfanyabiashara huyo Tinde na baadaye kumkamata dereva kumtuhumu kuwa alibeba magaidi kutoka Kahama hadi Shinyanga na baadaye kuwarudisha?

Suala la ugaidi linapotajwa kwa namna yoyote katika ardhi ya Tanzania, halina budi kufikiriwa kwa kina marefu na mapana hasa katika zama hizi za kujenga Uchumi ulio imara. Jambo hilo linaweza kukwamisha juhudi za serikali kwa kuwa watu kutoka mataifa mengine wanaposikia kuna ugaidi Tanzania, wanaweza kukatisha au kughairi azma zao ya kuwekeza nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tunapaswa sote kugeuka wamoja, chanjo kufikia wanajamii wetu wote

Na Yasmine Protace

**NI** jukumu la kila mlezi au mzazi kuhakikisha mtoto wake anapatiwa chanjo ambayo inatarajiwa kutolewa mwezi Juni mwaka huu.

Chanjo hiyo inawalenga watoto wote wadogo walio na umri chini ya miaka mitano. Kutolewa kwa chanjo hiyo kunamwezesha mtoto kuwa na ukuaji mzuri ambapo pia kutamfanya asipate magonjwa ya mara kwa mara.

Chanjo hiyo pia huimarisha kinga ya mwili ikiwamo afya ya macho ya watoto hao. Hapo, serikali kupitia Wizara ya Afya, imepokea vidonge vya matone ya Vitamini A milioni 22 kutoka kwa shirika la Nutrition International.

Hiyo ni kwa ajili ya kuwapatia watoto walio na umri chini ya miaka mitano wapatao milioni 11 kwa ajili ya kuongeza kinga ya mwili na kuimarisha afya ya macho kwa watoto hao.Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Mollel, anasema wakati wa makabidhiano ya vidonge vya matone ya Vitamini A kutoka shirika la Nutrition International jijini Dar Es Salaam.

Dk. Mollel anasema vidonge vya matone ya Vitamini A vitasaidia kuongeza kinga ya Mwili na kuimarisha afya ya macho kwa watoto walio na umri chini ya miaka tano.

Anafafanua kuwa elimu ya mtoto inaanza siku mimba inatunga na sio shuleni kwa kumpatia Mama lishe iliyobora wakati wa ujauzito ili kusaidia kuimarisha ubongo wa Mtoto

"Wazazi zingatieni lishe bora kwa watoto tangu wakati wa utungaji wa mimba na kuwa na desturi ya kula mlo bora kwa mama wajawazito na hii itamsaidia mtoto hata baada ya kuzaliwa na wakati yuko shule ubongo na akili yake kufanya kazi kikamilifu pia itampunguzia magonjwa ya mara kwa mara" Dk. Mollel anatamka.

Dk. Mollel anawataka Watanzania kuzingatia milo yao ya kila siku kwa kupata chakula chenye lishe hasa vyenye vitamini ili kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza kama shinikizo la damu , magonjwa ya moyo na kisukari

**Hiyo ni kwa ajili ya kuwapatia watoto walio na umri chini ya miaka mitano wapatao milioni 11 kwa ajili ya kuongeza kinga ya mwili na kuimarisha afya ya macho kwa watoto hao.**

"Hivi sasa watu wanakula kupitiliza na hawazingati chakula chenye lishe hivyo na kupelekea watanzania kusumbuliwa na magonjwa yasiyoambukiza kama uzito uliopitiliza, shinikizo la damu, magonjwa ya moyo na kisukari. Niwatake wahudumu wa afya ngazi ya jamii mkawape elimu watanzania waweze kutofautisha kati ya shibe na lishe",anasema.

Mtazamo wake ni, Serikali Awamu ya Sita ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, inatoa kiasi cha shilingi bilioni 99 kwa ajili ya kuajiri na posho za wahudumu wa afya ngazi ya jamii pia wamekuwa msaada mkubwa wa kufikisha elimu ya lishe na afya bora kwa jamii

Kwa upande wake Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete, ambae pia ni Mjumbe wa bodi ya menejimenti nchini ya shirika la Nutrition International (NI), anasema shirika tajwa limeipatia serikali vidonge vya matone vya Vitamini A milioni 22 kwa mwaka 22.

Pia akaongeza, kuwa vitamini A humsaidia mtoto kuimarisha afya ya macho na kuongeza kinga mwilini.

"Shirika la NI limetoa vidonge vya matone ya Vitamini A milioni 22 zitakazotolewa kwa awamu mbili, yaani mwezi Juni na Disemba kwa watoto takribani milioni 11 walio chini ya miaka mitano.

" Faida tano ya vitamini hivi ni kuimarisha afya ya macho na kuongeza kinga ya mwili kwa mtoto hivyo ni muhimu kwa wazazi kuhakikisha watoto wanapatiwa matone haya," akatamka mstaafu Kikwete.

# Madiwani, wenyeviti wa mitaa walipwa mabilioni na TAMISEMI

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imesema hadi Februari 2024, Sh. bilioni 13.5 zimetolewa kwa ajili ya kulipa posho za madiwani katika halmashauri 168.

Vilevile, Sh. bilioni 1.15 zimetolewa kwa ajili ya kulipa posho za wenyeviti wa vijiji, vitongoji na mitaa.

Naibu Waziri katika ofisi hiyo, Dk. Festo Dugange alibainisha hayo jana bungeni jijini hapa alipokuwa anajibu swali la Mbunge wa Mbulu Vijijini (CCM), Flatei Massay.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itawalipa posho wenyeviti wa vitongoji na vijiji na kuongeza posho ya madiwani ili kuwasaidia kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na wenyeviti wa vijiji, vitongoji na mitaa katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi.

"Serikali imeendelea kulipa posho za wenyeviti wa vijiji, vitongoji na mitaa ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao ipasavyo," alisema.

Naibu Waziri alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/24, serikali imetenga Sh. bilioni 1.7; hadi kufikia Februari, mwaka huu, Sh. bilioni 1.15 zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kulipa posho za wenyeviti wa vijiji, vitongoji na mitaa.

Pia alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24, serikali imetenga Sh. bilioni 20.8 kwa ajili ya kulipa posho za madiwani katika halmashauri 168 ambapo kufikia Februari, 2024 kiasi cha Sh. bilioni 13.5 kimetolewa.

Alisema serikali inaendelea kuongeza na kuboresha vyanzo vyake vya mapato ili kuendelea kulipa posho za madiwani, wenyeviti wa vijiji, vitongoji na mitaa.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema jimboni kwake wenyeviti wa vijiji na vitongoji hawajawahi kupata posho hizo ili kufanya shughuli zao, hivyo akataka kujua lini watalipwa.

Dk. Dugange, akijibu swali hilo, alisema serikali inathamini kazi za viongozi hao na imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuwagizia kumwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbulu Vijijini kuanza kutenga fedha kwenye mapato ya ndani kadri ya maelekezo ya sheria na miongozo.

Pia alisema serikali inaendelea kufanya tathmini kuangalia uwezo wake wa kifedha na itatoa tamko namna ya kushughulikia suala la nyongeza ya posho kwa madiwani.

# Mkopo ununuzi wa magari 150 ya Zimamoto waiva

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imearifu Bunge kuwa imekamilisha taratibu zote za mkopo wenye masharti nafuu wa Dola za Marekani milioni 100 kwa ajili ya ununuzi wa magari 150 ya Jeshi la Zimamoto na uokoaji pamoja na vifaa kwa nchi nzima.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda alieleza hayo bungeni jijini hapa jana alipojibu swali la Mbunge wa Temeke (CCM), Dorothy Kilave kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mbunge huyo alitaka kujua mpango wa swerikali kununua magari ya kuzima moto kwa ajili ya Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Mchicha, wilayani Temeke.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Pinda alisema mkopo huo ni kutoka Taasisi ya ADEX ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Alisema serikali imeendelea na jitihada za kuimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili litekeleze majukumu yake kwa ufanisi.

"Katika mwaka huu wa fedha 2023/24, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepata jumla ya magari 12 ya zimamoto na uokoaji yaliyopatikana kutoka katika mkopo wa Euro millioni 4.9 kutoka katika Serikali ya Austria ambayo yatasambazwa katika vituo vilivyoainishwa kikiwamo hicho cha Temeke,"alisema.

Naibu Waziri Pinda alitaja vituo vingine vitakavyonufaika ni pamoja na Ilala, Kinondoni, Dodoma, Mwanza, Morogoro, Mbeya, Arusha na Kilimanjaro.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji serikali itagawa lini magari hayo.

Naibu Waziri Pinda, akijibu swali hilo, alisema kati ya magari ambayo tayari yamewasili, yapo maalum kwa ajili ya kubeba maji ya dharura pindi gari la zimamoto linapoishiwa maji ili kuimarisha utoaji huduma ya kuzima moto.

Alisema magari hayo yanasubiri kuzinduliwa ndipo yagawanywe kwenye maeneo tajwa.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe akijibu maswali yaliyoulizwa na Wabunge kwenye kikao cha tatu mkutano wa 15 wa Bunge la 12, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Utafiti wa kusambaza gesi Dar nzima kukamilika Juni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Nishati kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kushirikiana na Kampuni ya TAQA Dalbit inafanya utafiti za mahitaji ya gesi asilia na njia za kusambazia katika Jiji la Dar es Salaam, ukitarajiwa kukamilika Juni 2024.

Naibu Waziri, Judith Kapinga aliyasema hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Kawe (CCM), Josephat Gwajima ambaye alihoji lini serikali itaweka mabomba ya gesi katika jiji hilo kila nyumba ili wananchi wapikie nishati safi na nafuu.

Akijibu swali hilo, Judith alisema hatua hiyo itawezesha kuwa na mpango madhubuti wa usambazaji gesi asilia utakaozingatia kero ya mipango miji katika jiji hilo.

"Utafiti huu utaonesha namna bora ya kufikisha mabomba na kuainisha maeneo yanayofaa na yasiyofaa kupelekewa mabomba ambapo njia nyingine zitatumika kuhakikisha gesi inafika kwa wananchi," alisema. Naibu Waziri Judith alisema serikali kupitia TPDC inaendelea na utekelezaji miradi mbalimbali ya usambazaji gesi asilia jijini Dar es Salaam.

"Hadi sasa serikali imeshasambaza gesi asilia kwa njia ya mabomba katika nyumba 880 katika Jiji la Dar es Salaam kwenye maeneo ya Sinza (226), Mikocheni (155), Kurasini (344) na Mwenge Mlalakuwa na Chuo Kikuu - UDSM (155),"alisema.


Pia alisema serikali imejenga bomba la gesi lenye urefu wa kilomita 12.4 kutoka Mwenge hadi Mbezi Beach kupitia barabara ya Bagamoyo.

"Bomba hilo lina matoleo katika maeneo mbalimbali ili kuweza kuunganisha wateja wa majumbani. Kwa kuanza tayari viwanda viwili na hoteli sita zimeshaunganishwa na bomba hilo katika eneo la Mbezi Beach na itaendelea kuunganisha wateja wa majumbani kwa maeneo yanayopitiwa na bomba hili,"alisema.

Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko alisema maeneo ya vijijini wamehamasika kutumia nishati safi lakini gharama ya ujazaji gesi ni kubwa na kuhoji mkakati wa kuweka ruzuku ili waondokane na matumizi ya kuni na mkaa.

Naibu Waziri Judith, akijibu swali hilo, alisema serikali inatarajia kukamilisha hivi karibuni mkakati wa nishati safi ya kupikia ili kukabiliana na vikwazo vinavyosababisha wananchi wasitumie gesi kupikia.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Biteko atangaza kibano watendaji TANESCO

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ametangaza kibano dhidi ya wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) huku akiweka bayana kwamba watendaji wazembe hawatavumiliwa kamwe.

Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Biteko ameagiza ripoti ya taarifa kila wiki ya Kituo cha Huduma kwa Wateja cha TANESCO ianze kutolewa ili kufahamu maeneo yenye changamoto ya umeme nchini na kurahisisha watendaji wazembe kuchukuliwa hatua kwenye maeneo hayo.

Dk. Biteko alitoa agizo hilo jana wakati wa ziara kwenye kituo hicho cha huduma kwa wateja jijini Dar es Salaam. Katika ziara hiyo, Dk, Biteko alitoa maagizo mbalimbali yenye lengo la kuongeza ufanisi wa kituo hicho muhimu kwa wananchi nchini. "Wateja wote wanaopiga simu kwa sababu mnaletewa matatizo ya wananchi ni lazima mtengeneze kila wiki tupate ripoti ni mkoa gani wanahudumiwa wateja kwa haraka na mkoa upi haupewi huduma kwa haraka ili tuchukue hatua," alisisitiza.

Aliagiza kila mkoa nchini uloko chini ya TANESCO ufanyiwe tathmini kujua umeme umekatika mara ngapi na kufahamu sababu zilizofanya kukatika katika maeneo hayo ili kama ni uzembe umefanyika serikali ichukue hatua haraka.

"Ninafahamu kuna wakati umeme unakatika si kwa sababu ya matatizo makubwa bali ni kwa matatizo madogo madogo ya kiusimamizi kwenye laini zetu. Unakuta kuna mahali mti umedondoka kwenye njia zetu na unachukua muda mrefu kuondolewa au mteja amepiga simu anachukua muda kuhudumiwa. Tunahitaji hiyo ripoti," alisema.

Dk. Biteko pia aliagiza kituo kuangalia utaratibu wa namna nzuri ya wateja kutogharamia malipo kipindi wanapopiga simu kuhudumiwa na kituo.

"Kiu yangu ni kuona tunakuwa na mfumo wa kupiga simu kwa wateja bila kuwaingiza kwenye gharama kwa sababu kuwaingiza kwenye gharama haina maana yoyote kwa wananchi," aliongeza.

Biteko alimwagiza meneja wa kituo hicho kuhakikisha taarifa ya maendeleo ya kituo hicho kwa kila mkoa inawasilishwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati ili kuongeza ufanisi wa watendaji nchini na asipofanya hivyo, atafanyiwa mabadiliko katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia sasa.

Vile vile, ameagiza TANESCO kujenga taswira nzuri ya nchi kupitia watendaji wake kupitia kituo hicho. Alisema Sh. bilioni 2.9 za dharuara zilizotolewa na serikali, ziwahudumie watu ili kufurahia huduma hiyo.

Agizo hilo la Biteko ni mfululizo wa kuhimiza utendaji na huduma bora ndani ya shirika ili kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa uhakika unakuwapo ili kuleta maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Februari 23, mwaka huu, Dk. Biteko alisitisha likizo za wafanyakazi wote wa TANESCO hadi mgawo wa umeme uliokuwa ukilikabili taifa unapatiwa suluhisho.

Naibu Waziri Mkuu Biteko alitoa agizo hilo alipotembelea kituo cha kuzalisha umeme cha Kidatu mkoani Morogoro na kubaini kuwa meneja wa TANESCO Mkoa wa Morogoro alikuwa likizo ilhali kuna mgawo wa umme.

Alisisitiza kuwa aliposema hakuna mfanyakazi wa TANESCO atakayelala hadi tatizo hilo lipatiwe ufumbuzi, alimaanisha kuwa kila mmoja awe kazini, hivyo akashangaa meneja huyo anakwenda kupumzika ilhali kuna tatizo la umeme nchini.

Aidha, usiku wa kuamkia Jumatatu, kulitokea hitilafu katika gridi ya taifa, hivyo kusababisha kukosekana kwa umeme katika maeneo mbalimbali nchini.

Kutokana na tatizo hilo, Biteko aliitaka TANESCO kutafuta suluhisho la kufeli kwa mfumo wa gridi ya taifa mara kwa mara, kwa kufanya upembuzi wa kina ili kuboresha miundombinu kwenye gridi hiyo.

Dk. Biteko alitoa maagizo hayo alipofanya ziara ya dharura katika mitambo ya kufua umeme ya Kidatu, mkoani Morogoro, kutokana na kufeli kwa mfumo wa gridi ya taifa, kulikosababisha mikoa mingi Tanzania Bara na Zanzibar kukosa umeme.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kushoto), akitazama namna Kituo cha Huduma kwa Wateja kinachosimamiwa na Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO), kinavyopokea simu na kuhudumia wananchi, alipokitembelea jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: WN**

# Watu 128 mbaroni tuhuma za kuuza nyara za serikali

**Na Neema Hussein,**
MPANDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi linashikilia watuhumiwa 128, akiwamo anayedaiwa kukutwa na koki 330 za mabomba, mali ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mpanda.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi, SACP Kaster Ngonyani, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana kuhusu utendaji wa jeshi hilo kwa mwezi Machi mwaka huu, alisema koki hizo ziliibwa kwa wateja waliounganishwa huduma ya maji na kuuzwa kama vyuma chakavu.

Alifananua kwamba watuhumiwa sita kati yao wamekamatwa na gunia moja na madebe mawili ya madawa ya kulevya aina ya bangi na kete 212.

Pia, Kamanda Ngonyani akafafanua kuna watuhumiwa 15 walikamatwa na pombe haramu aina ya gongo lita 223, huku wengine wanne wakidaiwa kujihusisha na matukio ya kujeruhi.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, watuhumiwa 84 pia wamekamatwa kwa makosa ya uzembe na uzururaji, watuhumiwa 10 walikutwa na mali za wizi ambazo ni viambaza (televisheni) vitatu, pikipiki mbili, redio (sabufa) tatu, mabati sita, baiskeli mbili vitanda viwili vya mbao, milango miwili ya vioo, sofa moja, feni na jokufu.

Alisema watuhumiwa sita wamekamatwa wakiwa na nyara za serikali vipande 40 vya nyama ya wanyamapori wanaodhaniwa kuwa ni swala na miiba miwili ya nungunungu.

Kuhusu kesi mahakamani, Kamanda Ngonyani alisema jumla ya watuhumiwa 28 walipatikana na hatia na kuhukumiwa vifungo mbalimbali, mmoja akihukumiwa kifungo cha miaka 20 gerezani kwa kosa la kupatikana na nyara za serikali, meno manane ya tembo.

Watuhumiwa tisa walifungwa miezi sita jela kwa kosa la kufanya shughuli za uganga bila kibali huku watuhumiwa 12 walihukumiwa kifungo cha miezi sita jela kwa kupatikana na pombe haramu (gongo).

Mtuhumiwa mmoja alihukumiwa miezi minane kwa kosa na kutoroka chini ya ulinzi, watuhumiwa wanne walihukumiwa miaka mitano kwa kupatikana na mali za wizi na mmoja alihukumiwa miezi sita kwa kosa la kutishia kuua kwa kutumia silaha.

Katika mapambano ya kuzuia ajali, alisema Jeshi la Polisi limewakamata madereva 2,326 kwa kukiuka sheria za usalama barabarani; watatu wamefikishwa mahakamani na kulipa faini huku wengine wakipewa onyo.

# Mkandarasi Mkuu wa SGR atoa msaada kituo cha kulea yatima

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Yapi Merkezi ambayo ni Mkandarasi Mkuu wa mradi wa reli ya kisasa (SGR) imetoa msaada kwa kituo cha kulea watoto yatima cha Mama Mwana kilichoko Vingunguti, jijini Dar es Salaam.

Msaada huo ni sehemu ya mkakati wa kampuni hiyo wa kujitolea kwa jamii, mchango huo ukilenga kutoa mahitaji muhimu kwa watoto wanaoishi katika kituo hicho wakati wa sikukuu zijazo za Eid El fitir.

Kampuni hio imetoa msaada wa bidhaa mbalimbali ikiwamo chakula, vifaa vya usafi, majokofu na nguo ili kuwapa faraja watoto hao katika kipindi cha sikukuu.

Amisa Juma, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano Yapi Merkezi, alitoa shukrani zake kwa kupata fursa ya kusaidia Kituo cha Watoto Yatima cha Mama Mwana.

Alisema "Yapi Merkezi ina nia ya dhati ya kuleta matokeo chanya katika jamii tunazofanyia kazi. Tunapokaribia msimu wa sikukuu ya Eid, ni jukumu na furaha kwetu kutoa msaada kwa kituo cha watoto yatima cha Mama Mwana na kuleta tabasamu kwenye nyuso za hawa watoto wanaostahili," alisema.

Amisa aliongeza zaidi, "Mchango wetu unaakisi tunu kuu za Yapi Merkezi ambazo ni ukarimu na uwajibikaji wa kijamii. Tunatumaini kupitia mchango huu, tunaweza kuwapa faraja na furaha watoto wa kituo cha Mama Mwana, huku tukiendelea kuwakumbusha kuwa wana haki ya kuthaminiwa na kutunzwa, pamoja na kuhimiza zaidi kampuni zingine za kiserikali na kibinafsi kuendelea kufariji jamii hizi."

Hafla ya kukabidhi msaada huo jana, ilihudhuriwa na wawakilishi kutoka mnejimenti na wafanyakazi wa kampuni ya Yapi Merkezi, wakiongozwa na Levent Doruck, Ofisa Mkuu wa Fedha wa kampuni iyo, ambaye aliwasilisha dhamira ya kampuni hiyo ya kuendelea kusaidia juhudi zinazoendelea za kuboresha mazingira ya watoto yatima au wanaoishi katika hali ngumu.

Mlezi Mkuu wa Kituo cha Mama Mwana, Saada Omar, alitoa shukrani na kupongeza kampuni ya Yapi Merkezi kwa moyo na ukarimu wao, huku akiendelea kusisitiza faida na umuhimu wa michango hiyo kwa ustawi wa watoto hao.

Yapi Merkezi imeahidi kuendelea kukuza ushirikiano na Kituo cha Watoto Yatima cha Mama Mwana, ikisisitiza dhamira yake ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii na mipango ya maendeleo ya jamii.

# Kiongozi wa Mwenge awavaa 'wajumbe' kuelekea uchaguzi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KIONGOZI wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Godfrey Mnzava, amewavaa 'wajumbe' ambao ni wapiga kura ndani ya vyama vya siasa, akionya wasidhani huu ndio wakati wao wa kuvuna fedha, kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji wa Mwaka 2024.

Mnzava amehoji wagombea wanaozitafuta nafasi za uongozi kwa njia ya rushwa, wanataka nini, na kwa nini atumie fedha nyingi kuingia madarakani.

Akizungumza jana na wananchi wa Kijiji cha Kimashuku kilichoko Kata ya Mnadani, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, alikokwenda kuweka jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa Zahanati, Kiongozi huyo wa Mbio za Mwenge Kitaifa, alitaka wananchi wasiruhusu vitendo vya rushwa

"Ukiona vitendo vya rushwa, tusiruhusu kwa sababu tutapata viongozi ambao hawana sifa, bali wana hela (fedha) mfukoni.

"Katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Vitongoji, tujiepushe na vitendo vyovyote vile vinavyoambatana na rushwa. Rushwa ni adui wa haki, rushwa ni adui wa maendeleo.

...Na katika chaguzi hizi mambo yamekuwa mengi kweli kweli. Wajumbe nao wanaona ndio wakati wa kuvuna. Hivi unakwenda kuvuna nini kwenye uchaguzi?

Na kwanini yeye anataka kuwa kiongozi akupe wewe hela ili aingie kwenye madaraka. Anataka nini huko?" Alihoji Mnzava.

Mwenge umekagua, kuweka jiwe la msingi na kuzindua miradi yenye thamani ya Sh. 995,725,202.

Miradi iliyozinduliwa ni uhifadhi wa chanzo cha maji Njoro (Kata ya Mnadani), ujenzi wa tangi la maji Rundugai (Kata ya Masama Rundugai) na ujenzi wa Zahanati ya Kimashuku (Kata ya Mnadani).

Mwingine ni ujenzi wa barabara ya lami Bomang'ombe, kilomita 0.3 kwa kiwango cha lami, mradi wa vijana wa ungenezaji wa samani kwa kutumia vioo na aluminium (Kata ya Bomang'ombe) na ujenzi wa shule mpya ya sekondari (Saashisha Sec-Kata ya Muungano).



Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Amos Shimba (kushoto), akielezea namna Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ilivyofanikisha utekelezaji wa ilani ya CCM ya jamii kupata huduma ya maji kwa asilimia 85 ifikapo 2025, wakati wa kikao cha wadau wa maji, wilayani humo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Malasusa awapa somo jipya watoa huduma afya

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Alex Malasusa, amewapa somo jipya, watoa huduma za afya nchini, akiwahadharisha kuacha kiburi na kufanya kazi kizembe.

Pia, amesema kufanya huduma hiyo kwa njia yoyote ile inayoonyesha kuna uzembe ndani yake, wanamuagusha Mungu aliyewaweka katika nafasi hiyo ya huduma kwa wahitaji.

Malasusa, aliyasema hayo baada kuitembelea Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini ya KCMC. Alisema KKKT inaamini kazi ya madaktari na wauguzi, ni kazi ya Mungu.

"Mungu amewaweka wanadamu kuwa mikono yake ya tiba, ndio maana kanisa letu linaamini kazi ya madaktari, kazi ya wauguzi, ni kazi ya Mungu. Wewe ni mkono wa Mungu, ukizembea umemuangusha Mungu," alisema Askofu Malasusa.

"Tunaona fahari, tunao mchango katika jamii ya Tanzania, hasa katika tasnia nzima ya afya, na si tu kutibu lakini pia, kufanya utafiti. KCRI ni taasisi inayojulikana Afrika, kwa kusheheni watafiti waliobobea.

...Lakini pia KCMC inajulikana sana kwa kuandaa madaktari; na madaktari wengi katika nchi hii wametokea hapa.

"Katika yale maono ya kwanza ilikuwa ni kutibu, kufundisha pamoja na kufanya utafiti; na hayo matatu mpaka sasa ndiyo yameendelea kubebwa na Shirika la Msamaria Mwema hadi leo."

Mkurugenzi wa Hospitali hiyo ya KCMC, Prof. Gilleard Masenga, alisema kwa sasa mpango mkakati wa KCMC, ni kutoa huduma za kibingwa na bingwa bobezi, kwa Kanda ya Kaskazini na Afrika kwa ujumla.

Alisema katika kutekeleza majukumu hayo yote, watatoa huduma za tiba, mafunzo pamoja na kufanya utafiti.

Pia, alisema utaratibu wa kutoa huduma hizo za kibingwa bobezi, unaendelea vizuri, ambapo ndani ya kipindi cha miaka mitano wameongezeka madaktari bingwa 60.

# Vijiji 46 vyanufaika mipango matumizi bora ardhi

**Na Oscar Assenga,** MKINGA

VIJIJI 46 vimenufaika na uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoja na vijiji 34 vimewezeshwa kupimwa upya mipaka yake kupitia mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi wilayani Mkinga

Mkuu wa Idara ya Ardhi wa Halmashauri ya Mkinga, mkoani Tanga, Emanuel Magembe, aliyasema hayo jana, wakati wa majumuisho ya mradi huo uliofadhiliwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na shirika la World Wide Fund (WWF) ulioanza tangu Oktoba 20, mwaka jana.

Alisema mradi huo umefanikiwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 46 (Village Land Use Plans) pamoja na kuimarisha mipaka ya vijiji kwa kupima upya mipaka ya vijiji 34 vya Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga.

"Utekelezaji wa mradi huu ulilenga kazi kuu mbili ambazo ni uimarishaji wa mipaka ya vijiji na uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji, tumefanikiwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 46, kupima mipaka ya vijiji 34, kusuluhisha migogoro 14 ya mipaka ya vijiji vilivyohusisha vijiji 26," alisema.

Aidha, alisema jambo lingine ni utoaji wa elimu ya sheria za ardhi na taratibu za umiliki wa ardhi kwa wananchi pamoja na kuwezesha ajira ya muda (vibarua) kwa vijana takribani 120 walioshiriki katika usimikaji wa mabango yanayoonesha matumizi ya ardhi iliyopangwa," alisema Magembe.

Hata hivyo, alisema kupitia kazi ya uimarishaji mipaka ya vijiji, timu ya watalaam ilifanya uhakiki wa mipaka kwa kuhusisha halmashauri za vijiji, wananchi na kamati ya usuluhishi wa mipaka iliyoteuliwa na halmashauri za vijiji na kupitishwa na mikutano ya vijiji husika na makubaliano ya mipaka ilifikiwa na mihtasari kuandikwa.

Pia, alisema kazi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 46 umekamilika kama ulivyopangwa na vilevile utungwaji wa sheria ndogo zitakazotumika kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi iliyoandaliwa.

Katika mpango huo vijiji vilivyonufaika na mradi huo ni Mwakijembe, Perani, Mkota, Mavovo, Mbambakofi, Kiumbo, Magati, Bwiti Mhinduro, Majengo, Muhezi, Churwa, Bamba Mavengero, Matemboni, Bombo, Mbuyuni, Vuga, Hemsambia.

Alivitaja vijiji vingine ni Kidundui, Machimboni, Mnyenzani, Jirihini, Vunde, Manyinyi, Kichangani, Mapatano, Mta kuja, Bantu, Sigaya, Kibewani, Bamba Mwarongo.

Pia, vipo Mzingi, Mwagogo, Msimbazi, Muzikafishe, Kwamtili, Kuze Kibago, Bosha Kwemtili, Mtoni Bombo, Kisiwani A, Kisiwani B, Ngombeni, Monga Vyeru na Kizingani.

Kadhalika vijiji vilivyofadhiliwa na Shirikaa WWF ni Mbuta, Mwakikonge, Mazola Kilifi, Dima, Mwanyumba na Magodi.





# Wahalifu tukio udhalilishaji mwanafunzi wasakwa

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Willbroad Mutafungwa, amemwagiza Mkuu wa Polisi Wilaya ya Nyamagana jijini hapa kufanya msako na kuwakamata watu wawili wanaotajwa kuhusika katika tukio la kumlawiti mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka 16 anayesoma kidato cha pili.

Agizo hilo lilitolewa juzi katika mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Jeshi la Polisi, Mkoa wa Mwanza na Kamanda Mutafungwa alisisitiza polisi washirikiane na wananchi kuwasaka wahalifu hao na kumtaka mkuu wa polisi wilayani hapo kubaki katika eneo hilo ili kutoa ushirikiano wa karibu zaidi kuwapata waliohusika kutekeleza kitendo hicho.

Alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Mwanza linatamani kuona wananchi wote wanafanya shughuli zao bila kuwa na hofu yoyote ya kufanyiwa vitendo vya ukatili na hilo lipo kwa ajili ya kusimamia usalama wa wananchi na mali zao.

"Mtu asishindwe kulima kwa sababu tu anaogopa kulawitiwa, kinachokosekana hapa ni ushirikiano wa pamoja kwa sababu nimemsimamisha Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa nikamuuliza sijaona kikundi cha ulinzi shirikishi hapa, naambiwa kwamba kikundi shirikishi ni cha siri hivyo hatuwezi kukubali kusumbuliwa na vijana wawili tena ni watoto wenu natoa maagizo yangu hao vijana wakamatwe vinginevyo hapa hapatatulia," alisema Mutafungwa.

Kijana aliyefanyiwa udhalilishaji huo alisema vijana hao wawili walimziba mdomo na kisha kumpeleka katika mlima wa mawe na kumfanyia kitendo hicho. Joyce Njagala, Mkazi wa Buguku alisema katika mtaa huo kumekuwa na matukio mengi ya kutisha, lakini serikali ya mtaa imekuwa dhaifu katika kuyachukulia hatua matukio hayo hivyo wameomba Jeshi la Polisi liwasaidie kwa kushirikiana na wananchi kukabiliana na matukio hayo.




Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda (wa tatu kushoto), akigawa msaada wa vitu mbalimbali kwa yatima baada ya futari iliyoandaliwa na Benki ya Azania, mjini Mugumu, wilayani Serengeti Mkoa wa Mara juzi. Kushoto ni Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Vincent Mashinji, Shekhe wa wilaya, Juma Simba (wa pili kushoto) na Mkurugenzi wa Maendeleo wa Benki hiyo, Dk. Rhino Nyansaho.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# OPD yajengwa miaka 10 bila kukamilika

**Na Neema Emmanuel,** SHINYANGA

WANANCHI wa Kijiji cha Singita, Kata ya Usanda, wilayani Shinyanga wameiangukia serikali kuwakamilishia ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) lililopo katika zahanati ya Usanda uliosimama takribani miaka 10.

Adelina Venance ni mkazi wa Kijiji cha Singita anaeleza kuwa wananchi wamejenga hatua za awali takribani miaka 10 iliyopita hatua iliyobaki ni ya serikali kumalizia na mpaka sasa hali ipo kimya na wao wakiendelea kuteseka na mrundikano wa wagonjwa katika zahanati hiyo.

Veronica Yakobo, amesema wanapitia wakati mgumu kwa sababu wagonjwa ni wengi pia wazazi wanachanganyikana na wagonjwa wengine jambo ambalo linawanyima uhuru na wanaomba kukamilishiwa kwa jengo hilo ili wapate huduma iliyo bora. Aidha, Mganga Mfawidhi wa zahanati ya Usanda, Hellen Kemi, alisema wanapokea wagonjwa takribani 600 hadi 800 kwa mwezi ikilinganishwa na hali halisi ya miundombinu iliyopo kwa kuwa kuna jengo lipo ameiomba serikali kulikamilisha ili kupanua ukubwa wa huduma.

"Kutokukamilika kwa jengo hili kunatupa wakati mgumu kwenye utoaji wa huduma kwenye kituo chetu tuna hudumia vijiji vitano pia tunapata na wagonjwa kutoka maeneo jirani na eneo letu ukweli kwa sasa miundombinu iliyopo haikidhi mahitaji kabisa wagonjwa ni wengi," alisema Kemi.

Akizungumzia suala hilo, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Dk. Nuru Yunge, aliishauri halmashauri kukamilisha ujenzi huo ambao wananchi wamemaliza kwa upande wao.

# Madiwani Iringa wafundwa ukusanyaji mapato

**Na Remmy Moka,** SAUT

MADIWANI wa Manispaa ya Iringa wamefundwa namna ya bora ya ukusanyaji wa mapato utakaowasaidia kukua kiuchumu katika halmashauri yao.

Elimu hiyo wameipata baada ya kufanya ziara ya kujifunza namna Serikali ya Mkoa wa Mwanza inavyokusanya mapato katika miradi mbalimbali na kuridhishwa na hali ya ukusanyaji mapato katika Halmashauri ya Manispaa Ilemela, jijini hapa.

Ibrahim Ngwada ni Mstahiki Meya wa Manispaa ya Iringa, alisema dhamira kubwa ni kujifunza namna Halmashauri ya Ilemela ilivyopiga hatua na mbinu wanazotumia kupata maendeleo kutokana na halmashauri hiyo kukusanya zaidi ya bilioni 11, ikilinganishwa na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ambayo inakusanya Shilingi bilioni nne.

Hellen Machibya mmoja kati ya madiwani wa Halmashauri ya Iringa, alisema walipendezwa na namna halmashauri hiyo inavyokusanya mapato na wanavyoboresha manispaa na madiwani wanavyosimamia mapato kwa ufasaha na kutumika kama inavyotakiwa pia wanavyotumia fedha za miradi katika kukuza uchumi wa halmashauri na mkoa kwa ujumla.

"Kupitia ziara hii itatusaidia kuwekeza nguvu kubwa ya namna bora ya kukuza pato katika halmashauri yetu kwani Mkoa wa Mwanza ni moja kati ya mikoa inayokuwa kwa kasi kiuchumi hivyo ni vizuri kujifunza namna ambavyo mkoa huu unavyokusanya mapato yake," alisema.

Aidha, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, Ummy Wayayu, alisema kupitia ziara hiyo wamejifunza mengi na kutoa wito kwa halmashauri zingine kuwa na utamaduni wa kutembelea maeneo mbalimbali ya nchi kwa lengo la kujifunza kwani ndiyo njia ya kupata maarifa mapya ya namna bora ya kukuza maendeleo ya nchini.



Ukurasa 12

Darasa wazoefu kwa vijana na kinamama, namna ya kufanikiwa katika soko la kimataifa




Ukurasa 13

Yawezekana kuwa na Mwenge wa Teknolojia mpya



Ukurasa 14

**Mafundi cherehani walivyo kundi muhimu, wakifunguka kiuchumi daima hawasogei**

BUFE
IJUMAA APRILI 5, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

UCHUMI

# Tabasamu Manyara, serikali kuwakomboa kutoka tabu za barabara, madaraja na taa

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MANYARA iko katika mikoa yenye mtandao mdogo kitaifa wa barabara za lami, ila ubora wa barabara zake unatajwa kuwa mzuri ukilinganisha na mingine, hata ukafanya barabara zake nyingi kusimamiwa na Wakala wa barabara Tanzania (TANROADS), zinapitika wakati wote.

Kwa mujibu wa Meneja TANROADS mkoa wa Manyara, Mhandisi Dutu Masele, hadi sasa wanasimamia mtandao wa kilomita 1,657 kati ya hizo kilometa 207 ni barabara kuu na zilizobaki 1,450 ni za mkoa.

Mhandisi Masele anafafanua, katika hizo kilomita 207, barabara kuu zote ni lami.

Aidha, anataja mkoa una madaraja 235, kati ya hayo 74 yapo barabara kuu na madaraja 161 yaapo barabara za mkoa.

Masele anasema katika serikali ya Awamu ya Sit, kumejengwa daraja la Magara wilayani Babati, hata kusaidia kuondoa tatizo la wanafunzi na watalii kushindwa kuvuka mto Magara.

Anautaja ulikuwa kikwazo msimu wa mvua, ikigharimu zaidi ya shilingi bilioni 12 na sasa wananchi wanapitisha mazao yao ya kilimo na watalii wanavuka kwenda Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara.

Anasema kujengwa daraja hilo, kumesaidia kukuza uchumi katika maeneo hayo, ikwamo ongezeko la watalii.

Mhandisi Masele anampa pongezi Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akitaja Barabara mpya ya kiwango chja zege, eneo la Mlima Magara katika barabara ya Mbuyu wa Mjerumani hadi Mbulu ni ukombozi mkubwa .



Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani, inayopita mlima Magara ambako TANROADS wanajenga kwa kutumia zege. **PICHA: JALIWASON JASSON**

"Sehemu hii ilijengwa kwa kutumia bajeti ya miradi midogo ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/22, 2022/23 na 2023/24,"anafafanua Mhandisi Masele, akidokeza manufaa yake ni kuboresha usafiri wa Babati kwenda wilaya ya Mbulu na kurahisisha shughuli za kiutawala na wananchi kusafirisha mazao.

Anataja mengine, ni azma ya Rais kukubali ijengwe barabara ya Mbulu hadi Kijiji cha Garbabi kilomita 25 katika barabara ya Karatu/Mbulu hadi Haydom kwa kiwango cha lami.

Mtaalamu huyo wa barabara anasema gharama ya mradi ni shilingi bilioni 35.171 na utajengwa kwa miezi 18 ikijumuisha miezi mitatu ya usanifu na maandalizi ya kazi, wastani wa malipo asilimia 20 amekwishapewa mjenzi.

Meneja huyo anasema ujenzi wa nyumba za wasimamizi wa mradi, ofisi pamoja na maabara ya vifaa vya ujenzi umekamilika kwa asilimia 100 na utekelezaji kwa ujumla umefikia asilimia 32.

Mradi mwingine anautaja ni ujenzi sehemu ya pili, Labay hadi Haydom kilomita 25, mkataba uliokwishatiwa saini Mei 19 mwaka kati ya serikali na mkandarasi, kampuni ya ujenzi ya Kichina, mradi ambao bado hajuanza kujenga, ila uktarajiwa kugharimu shilingi bilioni 42.271.

Pia, anaorodhesha miradi mingine ni: Sehemu ya ujenzi barabara Dareda Centr - Dareda Mission kilomita saba; Dareda - Dongobesh, kilomita 60, ukigawanywa kwa awamu mbili (Dareda Centre - Dareda Mission kilometa saba na Dareda Mission - Dongobesh kilometa 53.)

Anafafanua kunaharakishwa ujenzi kuanzia Dareda Centre -Dareda, Mission kwa kuwa ina idadi kubwa ya magari kutokana na uwepo wa hospitali, vyuo huduma za kijamii na tayari mkandarasi ameshapatikana na unatarajiwa kutiwa saini wakati wowote ukigharimu shilingi bilioni 9.882.

### KUFUNGUA FURSA

Anasema miradi hiyo itafungua fursa za kiuchumi kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa, itasafirisha vizuri mazao ya kilimo na kuingia mikoa ya Kaskazini kufanya utalii na kuliingizia taifa fedha.

Anasema nchi za Burundi, Rwanda, Uganda na Sudani, zitaweza kusafirisha mizigo yao kutoka Bandari ya Mombasa, huku zikinufaika na bomba la mafuta linalojengwa kupitia Tanzania.

Meneja anasema mradi wa uwekaji taa barabarani ni mradi ulioko endelevu katika maeneo yote ya miji kwenye barabara za mkoa na barabara kuu.

Anasema hadi kufika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2023/24 mkoa umefanikiwa kuweka taa 890 katika miji inayopitiwa na barabara zake za mkoa na barabara kuu.

INAENDELEA UK.12

BIASHARA

# Darasa la wazoefu kwa vijana na kinamama, namna ya kufanikiwa katika soko la kimataifa

• Kutunza siri biashara, tarehe za safari, usimamizi imara...



Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la Women in Social Entrepreneurship (WISE), Dk. Astronaut Bagile akifundisha wanawake wajasiriamali biashara kimataifa. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

**Na Beatrice Philemon**

INAPOZUNGUMZIWA biashara ya kimataifa, siyo wafanyabiashara au wajasiriamali wote nchini wenye ufahamu wa kutosha namna ya kuanza na kufanya.

Inaelezwa inapotakiwa kuanzishwa biashara ya kimataifa, inashauriwa kitaalamu uwezekano unaanza na malengo kwenye biashara hiyo.

Mdau mzoefu, Dorice Kanyimba, Ofisa Mtendaji Mkuu, kutoka kampuni ya Dorice La Bamba iliyopo wilaya ya Kinondoni, mkoa wa Dar es Salaam anasema:

"Kwa mfanyabiashara au mjasiriamali anayetaka kuanza kufanya biashara ya kimataifa (yaani kununua bidhaa kutoka nchi za nje na kuja kuuza Tanzania), kila mtu ana mwanzo wake na inategemea yeye anataka kuwa ni nani, jitahidi kubalance kazi na biashara, pia unachokipenda wewe ndicho uwafanyie wateja wako wakati unapofanya biashata.'

Pia, anataja mwanzo wa biashara ya kimataifa, kutafuta kitu au bidhaa ambayo 'inatoka' haraka, kisha inasimamiwa na mwenye biashara, dhana ya dhuluma na ukiukaji wowote ikiwekwa mbali. Uaminifu inachukua nafasi kwenye biashara hiyo.

"Biashara ni jicho, kuweni na kujiamini na kitu unachouza au unachokifanya kwenye biashara zako." anasema.

Pia, anataja hali ya kuwajali wateja, ni jambo muhimu sana kwenye biashara, muuzaji ajitahidi kuwa na lugha nzuri na rafiki kwa wateja, ifanyike mteja aone unamthamini na fahamu wateja wako wanachokitaka.

Lingine linatajwa ni kusikiliza maoni na ushauri wa wahusika, kuhakikisha inakamilishwa mahitaji yao na njia hii itasaidia kupata wateja wengi zaidi, kudumu katika biashara na biashara yako pia kukua.

Pia, anasema mtu akiwa mfanyabiashara au mjasiliamali, anapaswa kutomwambia mteja wake siri ya kazi zako au biashara yako.

Kanyimba anasema, mfanyabiashara au mjasiriamali akisafiri anapata faida ya kitu anachokifanya

Pia, kuna kufanyika biashara kwa ujasiri, kila mara mhusika akikumbuka kuwa ushindani ni mkubwa sokoni, ajitahidi kununua bidhaa zenye ubora kwa ajili ya wateja wako, kuongeza tija na ubora wa huduma kwenye biashara unayoifanya.

"Kila biashara inakabiliwa na changamoto, kamwe usikate tamaa kwenye biashara unayofanya, jitahidi sana kuwa jasiri kwa biashara unaofanya," anasema Kanyimba.

**ENEO LA USAFIRI**

Kanyimba anasema, wafanyabiashara au wajasiriamali wanaohitaji kuanza biashara ya kimataifa ya kununua bidhaa nchi za nje kama vile mashati, viatu, cheni, pochi, nguo za watu wazima, nguo za watoto na bidhaa nyingine na kuleta katika soko la Tanzania, kwenye eneo la usafiri China na Uturuki. Uturuki bei zipo juu na China bei zipo chini.

"Ukitaka kwenda China kununua bidhaa kwa ajili ya kuuza Tanzania, sasa hivi kuna makampuni mengi ya usafiri China, makampuni hayo yana masoko yote na ukitaka kununua bidhaa wanakupeleka kwenye soko.

"Na ukitaka kujua masoko yaliyopo utazungushwa na kampuni na usafiri wao. kwa hiyo naomba watanzania watumie fursa hii kwa sababu hivi sasa upatikanaji wa bidhaa nchini China imekuwa tofauti na miaka ya nyuma, anasema.

Mbali na hilo, inatajwa hadi sasa, usafiri kutoka Tanzania kwenda China nako sasa bidhaa nyingi hufuatwa na kuuzwa, kunatofautiana, gharama ya usafiri kutegemea na siku ya safari kwenda China.

**KUTOKA NGO**

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la kiserikali la Women in Social Entepreneurship (WISE), Dk. Astronaut Bagile, anasema mafunzo haya yalitolewa hivi karibuni na Kanyimba alipokuwa akizungumza na wanawake wajasiriamali kutoka Kisarawe (Pweni), Pugu, Sinza, Tuangoma na maeneo mengine ya mkoa wa Dar es Salaam na wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali.

Jumla ya wanawake wajasiriamali 45 waliojikita kwenye utengenezaji wa batiki, biashara ya vipodozi, ufugaji kuku, wabunifu wa majengo, biashara za nguo na unga wa lishe, utengenezaji wa keki, catering, wapambaji, magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo taasisi za mazingira walihudhuria mafunzo haya.

"Wakati wa mafunzo walifundishwa jinsi ya kuanza ulipo kwenda hatua nyingine, jinsi ya kuanza na kufanya biashara ya kimataifa, walipata nafasi ya kujifunza kutoka kwa wanawake wajasiliamali waliofanikiwa kwenye biashara ya kimataifa, hatua za biashara ya kimataifa na jinsi ya kununua hisa," anasema

Ni mafunzo waliopanda shirika lisilo la kiserikali la WISE kwa kushirikiana na Tanzania Child Welfare (TCW).

Anasema wameamua kutoa mafunzo kwa akina mama wenye umri tofauti tofauti na kada tofauti ili kuwasaidia vijana kujifunza kutoka kwao lakini pia waweze kupata maarifa na waone jinsi gani wanaweza kutumia maarifa hayo.

Mkurugenzi Mtendaji kutoka shirika lisilo la Kiserikali linaloitwa- Tanzania Child Welfare (TCW) Eddna Chandeu, anawashukuru wanawake wajasiriamali kushiriki mafunzo hayo na hatimaye kusaidia akina mama na vijana wa kike kujifunza vitu mbalimbali.

**UNUNUZI WA HISA**

Akizungumza kuhusu ununuzi wa hisa, Stella Anastazi, Oisa Habari kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), anashauri wananchi wote na akina mama wajasiliamali wanaopenda kununua hisa kutoka DSE au makampuni mengine kuzingatia masuala yafuatayo:

" Unapotaka kununua hisa lazima uwe na malengo, unaponunua hisa lazima ufuatilie kwenye kampuni ambayo umenunua hisa, ukibadilisha simu lazima uwafahamishe iili iwe rahisi kukupata na kupata taarifa.

"Pia, angalia nature ya kampuni unapokwenda kununua hisa, nunua hisa kwenye kampuni ambayo kila siku inatengeneza pesa, ukifika kwa 'broker' (dalali), jitahidi kumuuliza kuhusu dividend policy (sera ya hisa ), ili ufahamu kuwa kampuni yao inatoa gawio baada ya muda gani ili iwe rahisi kwako kuchukua maamuzi yaliyo sahihi katika ununuzi wa hisa," anasma.

Ligine la misistizo, anakumbusha mtu anapoibiwa isa aende katika Mamlaka ya Hisa, kwa sababu polisi wengi hawajui masuala ya hisa.

Anasema, pia hivi sasa mwanahisa anaweza kwenda kukopa benki kwa kutumia cheti cha hisa, akishauri wananchi na kinamama wajasiriamali wasiweke hela ambayo hawana matumizi nayo haraka.

"Wananchi wanaopenda kujifunza jinsi ya kununua hisa, faida ya ununuzi wa hisa, ununuzi wa hati fungani au bondi, CMSA inatoe elimu bure," anasema.

## Tabasamu Manyara, serikali kuwakomboa kutoka tabu za barabara

**INATOKA UK.11**

Anapataja kulikowekwa taa ni: Orkesumet, Mirerani, Kibaya, Endasak, Katesh, Bonga, Mbulu,Babati, Magugu,Dongobesh na Minjingu.

Pia, wakati Mkuu wa Kitengo cha Matengenezo TANROADS Manyara, Mhandisi Greyson Ndyamukama, anasema kujengwa daraja la Magara kumerahisisha mawasiliano ya watalii, wawekezaji mashamba makubwa na utawala wilayani Mbulu na Babati, kunAtajwa kumea kwa taa za barabarani.

Fundi Sanifu Mwandamizi na Msimamizi wa Usalama Barabarani, Elias Kajumam anasema serikali imesaidia kuwekwa taa za barabarani 688 mkoa mzima, kutoka 208 za zamani.

**WANANCHI WANAVYOITIKIA**

Diwani wa kata ya Magara, Jacob Elias, analitaja Daraja la Magara ni mkombozi na tegemeo lao wananchi.

Anantaoa ushuhuda tangu miaka ya 1970, hali ilikuuuwa mbaya kwa usafiri, eneo hilo wakati wa masika hivyo kujengwa daraja kunasaidia wilaya za Mbulu na Babati.

Anampongeza Meneja wa TANROADS kwa usimamizi wa barabara kwa kuwa msikivu akipigiwa simu hata kama ni usiku na kuambiwa matatizo ya barabara nyakati za masika tofauti na hapo anadai mvua zingewasumbua sana na kujikuta wamesimbwa na maji.

Mkazi wa Magara Roman Maswi, anasema kukamilika daraja hilo kumesaidia wanafunzi kuvuka kwenda shuleni kwa kuwa walikuwa hawaendi shule mvua ikinyesha.

Anamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kuridhia daraja lijengwe hivyo linawasaidia kuvusha mazao na kwenda kuyauza masoko ya Babati, Arusha na maeneo mengine.

Mkazi wa kijiji cha Bunyoda wilayani Mbulu Pristus Fanueli, naye anawakilisha shukurani zake kawekewa lami kutoka kijijini Garbabi kwenda Mbulu.

Fanueli anasema barabara hiyo ikikamilika itawawezesha kufanya biashara na bidhaa zao zitafuatwa na wafanyabiashara, huku akisema ataondokana na vumbi lililokuwa linajaa kwenye bidhaa zake.

Mkazi wa Mbulu, Loti Paul, anasema uchumi wao umekuwa chini kwa sababu ya barabara kutokana na mikoa kutokuunganishwa ila sasa mikoa itaunganishwa ikikamilika barabara ya Garbabi hadi Mbulu kuelekea Maswa.

Mkazi wa kijijini Njalanjala wilayani Mbulu John Josephath, anasema anaridhika na kasi ya ujenzi wa barabara hiyo kabla ya ujenzi anadai mvua ikinyesha makaravati yalikuwa yanakatika ila lami ndio itakomesha tatizo hilo.

**WAJENZI BARABARA**

Binti pekee Elizabeth Juma, aliyekutwa anajenga barabara ya Garbabi - Mbulu anaishukuru serikali kumuamini na kumpa kazi ya kujenga katia mradi huo.

Anasema kazi ya kujenga barabara inampatia maendeleo, akiwaasa vijana wenzake kufanya kazi kwa bidii bila kubagua kazi.


Pia John Sangu, anaishukru serikali kwa kuwaona vijana na kuwapatia kazi ya kujenga barabara anasema wanapata kipato tofauti na zamani walikuwa wanakaa vijiweni.

Hapo wanaungwa mkono na msimamizi wa mradi (Fomen) wa ujenzi wa barabara ya Garbabi-Mbulu Johanes Stephano, anakiri kazi kuendelea vizuri huku akiahidi kujenga kwa kiwango kinachotakiwa, kwa mujibu wa maelekezo.

Pia, msimamizi wa ujenzi wa barabara kwenye mlima Magara Kelvin Laxmidas, anaahidi kwa niaba ya makandarasi wazawa kuwa wataendelea kuwa waaminifu hivyo serikali ya iwapatie kazi, isiwatilie shaka.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Yawezekana kuwa na Mwenge wa Teknolojia mpya






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

JUZI kati nikapokea simu kutoka kwa mshikaji wangu wa siku nyingi tangu shule ya msingi. Baada ya kusalimiana na kujuliana hali, akaniambia yuko Dar anaishi Bunju.

Sikuamini nikamwuliza kwa nini hatuonani kama Jiji ni hili hili? Nikaamini kweli mji ni mkubwa na mambo ni mengi. Hivyo nikataka kujua nini zaidi baada ya salamu, akaniambia alikuwa na shida ya kupata taipureta!

Yawezekana vijana wa dot com wakawa hawajui ni kitu gani. Taipureta ni nini? Ni mashine ndogo inayotoa maandishi kama ya mashine ya kupigia chapa, lakini inayotumia ukanda maalumu wenye wino unaofanya herufi zilizogongwa zitokeze kwenye karatasi.

Wino huo ni mweusi na mwekundu. Baada ya matumizi ya muda mrefu, ukanda huo hupoteza nguvu na kutakiwa kuwekwa mwingine na ndipo taipureta huendelea kufanya kazi kwa maisha yake yote kutegemea na utunzaji wa mtumiaji.

Ofisi zilizoendelea enzi hizo, zilitumia taipureta kwa machapisho yake yote kuanzia barua, taarifa, mikataba na matangazo ya kiofisi na kulikuwa na makarani maalumu waliosomea kutumia kifaa hicho.

Taipureta ilishatoweka katika ofisi nyingi, hivyo nilishikwa na mshangao kumsikia jamaa yangu anatafuta taipureta, bila shaka nikawaza pengine alitaka kuitumia kichawi, kwa sababu haina kazi tena katika ulimwengu wa leo. Baada ya matumizi ya taipureta kukoma katika miaka ya baadaye ya tisini nchini, ziliingia kompyuta za vichogo, ambazo zilionekana kuwa zana bora na za kisasa wakati huo.

Ofisi iliyokuwa na kompyuta ilionekana kama ya Ughaibuni. Lakini, jinsi muda ulivyosonga mbele, zilikuja kompyuta zisizokuwa na vichogo; yaani kama luninga zilivyokuwa zikibadilika ndivyo na kompyuta zilibadilika kwa kuachana na vichogo.

Najua mpaka sasa ndugu yangu hajafanikiwa kupata taipureta hiyo, kwani haipatikani kabisa na bila shaka ziliteketezwa na kutumika kama chuma chakavu, kutokana na kumaliza muda wao wa matumizi.

Leo hii ukibahatika kuiona kwa mtu, basi pengine kaamua kuiweka kama makumbusho au anaitumia kwa shughuli za uganga, vinginevyo hazina matumizi kabisa. Sambamba na mabadiliko ya matumizi ya vitu, tunaona hivi sasa baada ya kuibuka simu za mkononi, hatuoni tena zile za mezani zilizokuwa zikitumika kwa kuzungusha kwa vidole, ingawa zipo za mezani za kubonyeza kama za mkononi.

Pia, simu za mkononi zimeua matumizi ya saa, zimeua kalenda na hata matumizi ya shajara. Wangapi hivi sasa wanategemea kupata muda kwa kuangalia saa mkononi?

Ndiyo sababu hata mafundi saa hawapo pia. Kwingineko hata matumizi ya redio za mezani yamekatika, kutokana na simu hizo hizo na kama zipo, basi ni mapambo na kujiburudisha kwa wale wapendao muziki mzito.

Ziko wapi hivi sasa treni zilizokuwa zikitumia kuni au magogo, zikiitwa magari moshi kutokana na moshi uliofuka kutokana na kuni hizo, lakini hata zilizokuwa zikitumia dizeli.

Hivi sasa tuna za umeme zisizochafua mazingira au tabaka la ozoni. Magari ya mafuta nayo polepole yanaanza kutoweka na nafasi kuchukuliwa na yanayotumia gesi na umeme, lengo ni hilo hilo la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuendelea kulinda ozoni.

Baadaye tutashuhudia hata nguzo za simu barabarani zikitoweka kutokana na matumizi ya simujanja zisizohitaji nyaya kuwasiliana, kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Yote hayo ni maendeleo ya teknolojia. Bila shaka tunaona hata kesi mahakamani zikiendeshwa kwa njia ya video. Wewe uko zako mahabusu lakini unawasiliana na hakimu aliyeko mahakamani kwingine kabisa, tena hata mikoani, inaitwa TEHAMA hiyo.

Hayo ni maendeleo ya kiteknolojia, yana faida na hasara zake; kukosa ajira ni hasara kubwa inayoletwa na mambo hayo, kuna akili mnemba inakuja, kuna matumizi ya maroboti yanakuja, hapo ajira itakuwa wapi ndugu yangu!

Lakini, kwa kuwa tumekubali teknolojia na kupeleka mambo kidijitali, hatuna budi kukubaliana na hali hiyo, ili tuweze kufikia maendeleo haraka kabla hatujarejea kwa udongo.

Ipo siku tutakapokubaliana na hali, tutajikuta tukishuhudia hata huu Mwenge wa Uhuru tunaokimbiza nchi nzima kumulika wabadhirifu walioshindikana ukisaidiana na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), nao unaboreshwa kuja na sura ya kisasa.

Kuendelea nao, basi inabidi uwe wa kisasa zaidi na wa teknolojia mpya, isiyotumia mafuta na badala yake utumie umeme, ili kuepusha uchafuzi wa tabaka la ozoni. Sawa tu na kuachana na treni ya dizeli na kuhamia kwenye umeme. Mnaonaje? Basi Kazi Iendelee!

BIASHARA

# Mafundi cherehani walivyo kundi muhimu, wakifunguka kiuchumi daima hawasogei

## • SIDO sasa kuwanoa, kuwakopesha mtaji

**Na Christina Haule,** Morogoro

HUDUMA ZA mafundi cherehani ni kongwe na ziko kila mahali nchini. Ila wenyewe wanalalamikia katika manufaa ya huduma hiyo, hawanufaiki na nyenzo za kiuchumi zinazowakweza.

Sasa wako katika maombi ya kusaidi kushona nguo wanapata mikopo itakayowasaidia, mitaji na ununuzi wa mashine za kisasa, hata ikarahisisha utoaji huduma kwa wateja, huku wakiongeza kipato kwa maendeleo yao na taifa.

Mwalimu wa Cherahani na Ushonaji Nguo kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda vidogo (SIDO) mkoani hapa, Isack Maufi, anasema mafundi wengi wa nguo wako chini kiuchumi.

Anafafanua wanaishi katika nyumba za kupanag, hawana magari na hawadhamiki kwa mikopo wanayoihitaji.

"Unapozungumzia suala la mitaji, bado gumu kwa mafundi nguo, kwa sababu hatuna thamani inayohamishika na kutuwezesha kupata mikopo," anasema Maufi.

Akirejea uzoefu wake wa miaka 20 kwenye ufundi cherehani na kushona, bado hajafanikiwa kufikia miliki hizo, kikuu wanaishia kujikimu na kisaiodai ndugu wa karibu.

Fundi huyo anasema, wakiwa na mashine za kusukuma kwa mguu kila siku, huwaondolea kujiamini, hawavutiwi na kazi zao, pia hawawezi kufanikiwa, bali mashine za umeme ndizo zinawawezesha kuendelea.

Katika hilo, anwaasa mafundi wenzake kujiunga katika vikundi hata inakapotokea nafasi wao kukopeshwa mitaji mikubwa, inakuwa rahisi wakainuka kiuchumi na kuboresha maendeleo, kama mafundi wengine aina yao wanavyoinuka.

Anaeleza wakipata mitaji mikubwa itawawezesha kununua vifaa vya kisasa, majora ya vitambaa, kufungua au kukodi fremu za biashara, kushona nguo na watakazoziuza kwenye magulio na masoko makubwa, wakajiongezea kipato.

"Mshonaji anaweza kuwa na mawazo makubwa kwamba anunue mashine ya umeme ambayo ni rahisi, lakini suala la mtaji ndio humfanya kubaki akitumia mashine za kusukuma na miguu, ambayo humchukua muda mrefu kukamilisha kushona nguo moja, tofauti na akiwa na mashine ya kisasa ya umeme ambayo humuwezesha kushona hata nguo tatu kwa siku" anasema Maufi.

Pia, anataja mikopo mikubwa



Baadhi ya mafundi Cherahani katika ofisi ya pamoja, eneo la Dumila, wilayani Kilosa wakishona nguo. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**

kwa mafundi kushona ina nafasi kuinua taaluma ya ushonaji nguo, hata kuwafanya mafundi chipukizi kuziona chachu za kazi yao.

Anasema, kazi inapokuwa nzuri inapaswa kukimbiliwa hata na vijana, katika nyakati zilizopo kukabiliana na wimbi wa ukosefu wa ajira nchini.

Maufi anasema, vijana wanaoanza kazi wakitoka mafunzoni, ni kundi ambalo likipatiwa mikopo, wanamudu kukwea kujiongezea ujuzi, katika uandaaji bidhaa za kufikia sokoni.

"Fundi chipukizi wa sasa anapaswa kukua kila siku na kutokuwa fundi chipukizi wa kizamani, ambaye alibaki kila siku kutoa mashine yake moja nje kwenye kibaraza chao ambayo wakati mwingine haina hata nyuzi za kushonea.

"Hali hii huwafanya mafundi chipukizi wengi kukata tamaa na kujiunga kufanya kazi viwandani, wakiamini watapata fedha nyingi tofauti na walipo," anatamka.

### AIPONGEZA SIDO

Maufi anaipongeza SIDO kwa kuona umuhimu wa kutoa elimu ya ushonaji wanafunzi 34 wa kike, akimini wanapokamilisha mafunzo hayo ya miezi mitatu, wanakuwa nafasi kubwa ya kujikita kwenye soko la ushonaji.

Pia, Maufi anatumia fusra hiyo tajwa, akiomba serikali ishiriki katika uingizaji mashine za chereheni umeme nchini, zenye gharama nafuu, tofauti na zilizopo sokoni sasa.



Mwalimu wa Cherahani, Isack Maufi (kushoto), akimuelekeza jambo mmoja wa wanafunzi 34 wanaopata mafunzo kupitia SIDO, mkoani Morogoro.

"Cherahani ya umeme moja ikiingia nchini huuzwa hadi shilingi laki saba hadi shilingi milioni moja," anasema Maufi.

Vilevile, anaiomba serikali kuangalia suala la kuboresha na kuimarisha upatikanaji umeme, ili kuwezesha uhakiki wake, ikifanikisha maendeleo ya viwanda nchini.

### DARASA ALIYEFANIKIWA

Rehema Sambui, mwanamke aliyefanikiwa katika ushonaji nguo, akitokea Kata ya Dumila wilayani Kilosa mkoani hapa, anaishukuru SIDO kuwapa mafunzo ya ushonaji wao watu 20, ikiwapatia cherahani kila mmoja.

Anasema baada ya kupata cherahani hiyo, mwaka 2021 wakafungua ofisi zao na wakaunda kikundi walichokiita 'Tujitume' chenye watu 18.

Rehema anaeleza, wakafungua ofisi tatu, ikiwamo ya kushona mabegi ya mapambo na kushona nguo za kawaida za maharusi. Katika ufafanuzi wake, anasema nje ya kikundi ana ofisi binafsi yenye mashine nane, huku akiwa na vijana aliowaajiri zaidi ya 10, anaowalipa kila mwezi kwa mapatano tofauti.

Anasema ufundi unamsaidia kuendesha familia yake huku akiwa na mtoto mmoja na wazazi wake na wadogo zake ambao wanamtegemea.

Hata hivyo kuhusu masoko, mama huyo ana ufafanuzi kwamba, SIDO imewasaidia mafunzo cherahani na elimu ya masoko, hivyo imewawezesha kuomba na kupata tenda kupitia kwenye shule za serikali na watu binafsi.

Kwa mujibu wa Mama Rehema, ni hali inayowainua kiuchumi, ikiendana na mabadiliko ya mtaji kiuchumi, ikilingainishwa na nyuma walipoanza ufundi.

### MENEJA SIDO

Hadi sasa, Meneja wa SIDO mkoa wa Morogoro, Joan Nangawe, anasema shirika lake linasambaza teknolojia ya msingi, mafunzo na kuwezesha wajasiriamali kupata masoko na mitaji, huku wakianzisha kituo maalum cha mafunzo na ubunifu kuwasaidia vijana.

Anasema kuanzishwa kwa kituo kumesaidia kuwawezesha wajasiriamali wanaochipukia kupata huduma ya teknolojia, ikiwamo mashine ndogo wahusika wakipewa mafunzo na zinatumika kama vitendea kazi.

Meneja Nangawe anasema, wameanzisha huduma ya kujifunza ujuzi wa kutengeneza vyerehani na kufundisha ushonaji nguo, ili kuwawezesha wahitaji kuzalisha vitu vitakavyokidhi mahitaji ya soko.

Kukitajwa sasa wameshaanza na wanafunzi 34 wakaotapewa cherehani za ruzuku kila mmoja watakapomaliza mafunzo, yatakayodumu kwa kipindi cha miezi mitatu.

Nangawe anaeleza mategemeo ni kuyaona matokeo mazuri kwa wanafunzi, baada ya mafunzo kukamilika, ili kuimarika kiujuzi na kukabiliana na changamoto za kimaisha ikiwamo ukosefu wa ajira.

Anarejea kwamba kituo hicho kimeanzishwa tangu mwaka 2023, kikishirikiana na SIDO Mkoa Mwanza kukiwapo wanafunzi 20 kutoka eneo la Dumila, Kilosa, waliofundishwa.

Baada ya hapo, wakakabidhiwa cherahani za ruzuku za shilingi milioni mbili, kuwezesha ushonaji kisasa na wenye manufaa kiuchumi.

Nagawe anasema, wanatazamia kila robo ya mwaka wawe na wanafunzi 30, hata mwisho wa mwaka wawe wamewaelimisha vijana 120 katika fani mbalimbali za ushonaji.

Hapo anataja ushonaji mavazi ya kike, kiume na zingine kama sherehe, mapambo ya nyumbani vitambaa na mashuka, wanaofunzwa kuvshwa kutoka hatua moja hadi nyingine, bila ya gharama kimitaji.

Hivyo, anawataka vijana wasibweteke kukaa nyumbani, bali wahakikishe wanapata mafunzo ya fani ili kuimarisha ujasiriamali wao.





# Mpango maendeleo sekta elimu waanza kufumuliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeanza kufumua mpango wa maendeleo ya sekta ya elimu 2021/22 -2025/26 ili kuendana na mabadiliko ya sera na mitaala mipya ya mwaka 2023 na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika ndani ya miezi sita.

Aidha, maboresho ya mitaala kwa ngazi ya elimu ya kati na juu yameanza ili kuwa na vijana wenye umahiri na ujuzi utakaowasaidia kujiajiri na kuajirika ndani na nje ya nchi.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa mwaka wa pamoja wa tathmini ya sekta ya elimu 2023/24, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Carolyne Nombo, alisema kazi hiyo inafanywa na wataalamu wabobezi kutoka ndani na nje ya nchi na kushirikisha wadau wa elimu.

"Wizara imeanza kusafisha mpango huu kwa kuzingatia mabadiliko ya sera na mitaala na matokeo ya sensa ya watu na makazi 2022, niwahakikishie kuwa wataalamu hao watayafikia makundi yote na tunatarajia kazi hii itakamilika mwezi Septemba 2024, na UNICEF ndio waratibu wa mapitio ya mpango wa maendeleo ya elimu," alisema.

Alisema wizara inaendelea mapitio ya nyaraka na programu mbalimbali zinazotumika kutekeleza sera na mitaala mipya toleo ya 2023.

Alifafanua kuwa serikali imefanya mageuzi makubwa ya mapitio ya sera ya elimu ya mwaka 2014 na kwasasa ipo sera ya elimu na mafunzo 2014 toleo la 2023 na mitaala mipya ya elimu ya awali, msingi, sekondari na mafunzo ya ualimu.

"Sera ya Elimu na Mitaala ndio nyenzo mama katika utoaji wa elimu nchini, niwahakikishie kuwa zimefanyiwa kazi kwa weledi mkubwa na wakuzingatia mazingira yetu na hitaji la soko na zitawasilishwa kwa kina katika mkutano huu," alisema.

Alisema kupitia mkutano huo wadau watajadili sera na mitaala hiyo ili kupata namna bora ya utekelezaji wake.

Naye, Mkuu wa Kitengo cha Elimu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Tanzania, Daniel Baheta, alisema kwa mwaka 2021, Tanzania ilionekana kuwa na upungufu mkubwa wa walimu hususani wa hisabati, lugha na sayansi na kuwa njia ya kukabiliana na hilo ni vyema kuwekeza katika teknolojia ambayo itasaidia kuweka daraja la ujifunzaji na ufundishaji.

Alisema Unicef na wadau wa maendeleo wataendelea kuisaidia Tanzania kifedha vipambele vya serikali vyenye lengo la kuboresha sekta ya elimu.

Awali, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Prof. James Mdoe, alisema washiriki wa mkutano huo watajadili mipango mbalimbali iliyofanyika kwenye sekta ya elimu ikiwamo sera ya elimu na mitaala na kuweka mikakati ya utekelezaji wake.



Mbunge wa Viti Maalumu Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ester Bulaya akichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## TET yakabidhi zaidi ya vitabu 20,000 shule awali

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

SERIKALI kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) imekabidhi vitabu 20,471 kwa ajili ya darasa la awali,la kwanza, tatu na mihtasari ya darasa la tatu hadi la saba katika shule za msingi 93 zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Asia Messos, akimkabidhi vitabu hivyo jana Mkuu wa Idara ya Elimu ya Awali na Msingi, Jusline Bandiko, alisema vitabu hivyo vina thamani ya Sh. milioni 24.

Messos aliishukuru serikali kupitia TET kwa kutoa vitabu hivyo na kwamba hizi ni juhudi za kuboresha elimu nchini.

Alisema shule ambazo zitapata mgao huo wa vitabu ambazo ni pamoja na Shule ya Msingi Maelu, Nduguti, Kidarafa, Miganga, Kinampundu, Ibaga, Lukomo, Kinyanguri, Ipuli na Msiu zihakikishe zinavitumia kufundishia wanafunzi kulingana na maelekezo waliopewa na serikali.

"Tumepokea vitabu 20471 kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) hizi zote ni juhudi za serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan katika kuboresha miundombinu ya elimu sambamba na mazingira ya kujifunzia na ufundishaji na vitainua taaluma katika wilaya yetu," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa walimu kuhakikisha vitabu hivyo wanatumia kwa ajili ya kufundishia wanafunzi na kwamba wakaguzi watakapopita shuleni kukagua wasikute vimewekwa kwenye makabati.

Naye Mkuu wa Idara ya Elimu ya Awali na Msingi, Jusline Bandiko, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuleta vitabu ili kupunguza upungufu uliopo na kuwawezesha watoto kujifunza kwa urahisi.

Vitabu vilivyotolewa kwa darasa la awali ni vitabu 6,836, darasa la kwanza vitabu 7,932 na darasa la tatu vitabu 5,703 na mihutahasari 1,378.

# Kampuni SUMA JKT zasaidia kuchangia pato la taifa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, amesema tangu kuanzishwa kwa shirika la SUMA JKT mwaka 1981, kumesadia kuchangia pato la taifa kupitia uzalishajai mali na kulipa kodi stahiki kupitia kampuni zake tanzu na miradi mbalimbali.

Dk. Tax amebainsha hayo jana jijini Dodoma, alipokuwa akitoa taarifa ya mafanikio ya wizara yake katika kipindi cha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema, pia limesaidia kuongeza ajira zilizo rasmi na zisizo rasmi 36,479.

Lengo kuu la kuanzishwa kwa SUMA JKT, ni kufanya biashara na kuzalisha faida ili kuchangia gharama za uendeshaji wa shughuli za JKT na kujenga uchumi wa taifa.

"Tangu kuanzishwa kwake JKT kupiti SUMA JKT imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na huduma kupitia sekta za ujenzi, uhandisi na ushauri, kilimo, mifugo na uvuvi, viwanda huduma na biashara," alisema.

Aidha, alisema shirika hilo limeshughulika na miradi ya kimkakati kama ujenzi wa Ikulu ya Chamwino Dodoma na taasisi nyingine nyeti nchini.

Kadhalika, alisema katika kipindi cha miaka 60 ya Muungano Jeshi la Wanachi wa Tanzania (JWTZ) limefanikiwa kuwezesha taifa kuwa na uchumi imara kutokana na kulinda amani na utulivu uliopo.

Alisema hali hiyo imesaidia wananchi kuendelea kufanya shughuli zao za uzalishaji mali bila kuwapo kikwazo.

"Katika kipindi cha miaka 60 ya Muungano jeshi letu limekuwa msaada mkubwa katika kusaidia ulinzi wa amani yetu pamoja na kulinda Katiba yetu hali ambayo imesadia kuwa na uchumi imara," alisema Dk. Tax.

Aidha, ili kuimarisha Jeshi hilo serikali kupitia wizara yake imeendelea kuboresha maslahi kwa wanajeshi na watumishi wa umma kadri uwezo wa kifedha unavyoruhusu ikiwamo kuwapatia makazi bora.

"Kuwajengea nyumba, pamoja na stahili mbalimbali, kupandisha vyeo kulingana na sifa, vigezo na taratibu," alisema.

Alisema hadi sasa serikali imejenga nyumba katika kambi mbalimbali za jeshi kwenye mikoa ya Arusha, Dar es Saalam, Dodoma, Kagera, Kigoma, Morogoro, Mwanza, Pemba, Pwani, Rukwa, Tabora na Tanga.

Alisema, ujenzi wa nyumba hizo umepunguza uhaba pamoja na changamoto zitokanazo na wanajeshi kuishi uraiani.

Alisema, mchango mwingine wa jeshi hilo katika miaka 60 ya Muungano ni ulinzi madhubuti wa mipaka, uhuru, na Katiba hali ambayo imesadia nchi kuendelea kuwa imara na yenye amani katika awamu zote.

Mafanikio mengine ni ushiriki wa wizara kupitia taasisi zake husani JWTZ, katika kukabiliana na majanga au maafa mbalimbali yanapotokea.





# H'shauri yahimiza elimu ya lishe bora, mifumo ya chakula

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imewasihi wadau na taasisi mbalimbali kujikita katika kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa lishe bora na mifumo ya chakula.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, John Nchimbi alitoa rai hiyo juzi wakati akizungumza kwenye warsha ya kujadili masuala ya lishe jijini hapa.

Alisema kuna kila sababu ya kujikita katika kutoa elimu na kubuni mbinu zitakazowezesha na kuhamaisha jamii kuzingatia lishe bora.

"Watoto wakipata lishe itawawezesha kuwa na afya bora kiakili na kimwili kwa kuwa wabunifu na wavumbuzi na hatimaye kujenga taifa lenye wataalam watakaoweza kusimamia vyema maslahi na maendeleo ya nchi," alisema Nchimbi.

Mganga Mkuu wa Jiji la Mbeya, Dk. Yesaya Mwasubila alisema kuwa hali ya lishe kwa sasa siyo mbaya na hivyo kuwapongeza walimu kwa kuthubutu kuzungumza na wazazi juu ya uchangiaji wa huduma ya utoaji chakula shuleni.

Ofisa Lishe Jiji la Mbeya, Itika Mlagalila alibainisha athari zinazoweza kujitokeza iwapo jamiii itakosa lishe bora akisema ni pamoja na kushuka kwa kiwango cha uzalishaji mali kwakuwa jamii itakuwa inajiuguza badala ya kufanya shughuli za uzalishaji.

Judith Sarapion kutoka Shirika la Helvets ambalo ni mwezeshaji wa mifumo ya chakula jijini Mbeya, alisisitiza kuzingatia utoaji wa elimu ya lishe kwa makundi yote kuanzia watu wazima, watoto waliopo shuleni na vijana ili kuwa na uelewa wa pamoja.

Hata hivyo Mwalimu Bether Gerald kutoka Idara ya Elimu ya Msingi Jiji la Mbeya alisema kuwa miongozo ya elimu imeeleza kuwa ni wajibu wa mzazi kuchangia chakula pia ni haki ya mtoto kupata chakula akiwa shuleni.

Alisema mpaka sasa asilimia 44.8 ya wanafunzi wa shule za sekondari za serikali wanapata chakula shuleni baada ya wazazi wao kuchangia chakula.

# Ubovu barabara wakwamisha malori 25 kutoka Mgololo

**Elizabeth John,** NJOMBE

MAROLI zaidi ya 25 yamekwama kwa zaidi ya siku tano katika kijiji cha Nyamande na Kitandiliko wilayani Njombe kutokana na ubovu wa barabara uliosababishwa na mvua.

Wakizungumza na waandishi wa habari, madereva hao wamesema changamoto kubwa katika eneo hilo ni wakala wa barabara kuweka kifusi chenye tope na kusababisha magari kukwama.

Walisema hawajui sababu haswa ya serikali kushindwa kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami ama changarawe kwani imekuwa na mchango mkubwa kiuchumi.

Mmoja wa madereva hao, Godwin Ngajilo alisema barabara hiyo inatumiwa na nchi zaidi ya tano ikiwemo Kenya, Uganda, Burundi na Zambia ambazo zinategemea karatasi kutoka kiwanda cha Mgololo.

"Tumejaribu kila namna imeshindikana hatuoni kiongozi yeyote hata kutupa msaada, sasa hivi tupo hapa na hakuna chakula mahali pa kufuata chakula ni mbali pikipiki ni Sh. 5,000 hadi Sh. 10,000," alisema Ngajilo.

Naye Jumanne Hussen alisema adha hiyo imesababisha watumie gharama kubwa kwa ajili ya kupata chakula na kueleza kuwa mpaka sasa hakuna kiongozi wa serikali ambaye amefika katika eneo hilo.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Kitandililo, Obedi Msingwa alisema kutokana na barabara hiyo kutopitika kwa zaidi ya siku tano kumesababisha abiria wanaotoka Mufindi kuishia Kitandililo.

Diwani wa Kata ya Kitandililo, Imani Fute alikiri kutokea kwa changamoto hiyo na kueleza kuwa barabara hiyo ipo chini ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Iringa na kufafanua jitihada za kutatua adha hiyo zinaendelea kwa kuwasiliana na viongozi wa wakala wa barabara na mbunge wa Mufindi.

Meneja wa TANROAD Mkoa wa Iringa, Yudas Msangi alisema hali hiyo imesababishwa na mvua ambazo zinaendelea kunyesha, kwamba wataifanyia marekebisho pindi mvua zikipungua.




Rais Samia Suluhu Hassan akikabidhi cheti cha usajili kwenye Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kwa Mkurugenzi wa kitengo cha Sheria wa Kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, Olaf Mumburi baada ya kuzindua tume hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake Mwalusembe wapewa msaada mitungi ya gesi

**Na Mwandishi Wetu**

BALOZI wa heshima wa Shelisheli nchini Tanzania, Maryvonne Pool kwa kushirikiana na Kampuni ya Oryx Gas, wamegawa mitungi ya gesi 400 kwa wanawake wa Kata ya Mwalusembe huku wakihimizwa kutunza mazingira kwa kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi mitungi hiyo, Balozi Maryvyonne Pool ambaye pia ni mwanzilishi wa taasisi ya African Reflections Foundation, alisema uamuzi wa kushirikiana na oryx kutoa mitungi hiyo kwa wanawake wa vijiji vya kata vya Mwalusembe, unatokana na kutambua na kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuhamasisha nishati safi ya kupikia.

"Hii kwangu si mara ya kwanza kwani mwaka 2022 nilinunua mitungi ya gesi na kugawa kwa wanawake wa Mkuranga kwa sababu mimi ni balozi wa heshima. Ndio maana nimekuwa nikishiriki katika miradi ya maendeleo ukiwemo wa kilimo cha kisasa cha umwagiliaji," alisema.

Alisema taasisi yake imekuwa ikiwasidia wanawake na vijana kulima, huku akibainisha kuwa hatua hiyo imetokana na kutambua mchango wa Rais Samia baada ya kuwa kinara wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi. Mkuu wa Wilaya Rufiji, Meja Edward Giwele, alisema umefika wakati wa kumuunga mkono kwa vitendo Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia kuokoa mazingira na kutanua fursa za kiuchumi hususani kwa wanawake wa wilaya hiyo na maeneo mengine nchini.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Janeth Rutashobya, alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa azma yao ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Alisema kampuni hiyo tangu Julai mwaka 2021, imejikita kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan kuhamasisha nishati safi ilijua kuwa kufanya hivyo kuna tija kubwa kwa jamii. Alisema miongoni mwa faida za kutumia nishati safi ni pamoja na kuokoa muda mwingi uliokuwa ukitumika kupika chakula kwa kuni au mkaa.

Tawala Wilaya ya Mkuranga, Omar Mwanga, alisema wilaya hiyo ni miongoni mwa waathirika wa uharibifu wa mazingira.

# Vijiji sita Ludewa vyazingirwa maji, barabara yakatika

**Na Elizabeth John,** LUDEWA

VIJIJI zaidi ya sita wilayani Ludewa mkoani Njombe, vimeathiriwa na mvua baada ya maji kuingia katika makazi yao, huku mawasiliano ya barabara yakikatika pamoja na mazao ya chakula kusombwa.

Akizungumza na Nipashe mkazi wa Kijiji cha Kipingu, Grace Haule aliomba serikali iwasaidie chakula pamoja na sehemu za kukaa kwani mashamba yao yamesombwa na maji, huku baadhi ya nyumba zikititia na nyingine kujaa maji. Katibu Tarafa ya Masasi, George Kapongo alisema mvua hizo zimenyesha maeneo ya milimani na hivyo kujaza maji katika Mto Ruhuhu, Kipingu na kwenye mashamba ya watu.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga aliyefika katika vijiji hivyo, aliwapa pole wananchi hao na kuwataka kuwa watulivu wakati serikali ikijipanga kuwasaidia.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ludewa, Gervas Ndaki alisema chama kitaielekeza serikali ili iweze kutimiza baadhi ya majukumu yake ikiwemo mradi wa umeme pamoja na umwagiliaji ambao utapunguza kasi ya maji kwenda kwenye makazi ya watu.

"Mimi nimshukuru sana mbunge wetu amekuwa anahimiza na tunayo miradi mingi sana ambayo amekuwa akihimiza katika wilaya yetu ya Ludewa ikiwemo huu mradi wa umwagiliaji," alisema Ndaki.

Ndaki aliwataka wananchi kuchukua tafadhali hasa za kiafya kwa kutokunywa maji bila kuchemsha kwani kipindi cha mafuriko akisema kuna hatari ya kuibuka magonjwa ya mlipuko hasa kipindupindu.





## Wakurugenzi sera, mipango watakiwa kuzingatia usawa kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Abeidah Rashid Abdallah amewataka wakurugenzi wa sera na mipango katika wizara za Serikali kuzingatia usawa wa kijinsia wakati wanapoandaa bajeti zao.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua kikao cha kuwajengea uwezo wakurungezi wa sera na mipango na baadhi ya maofisa wadhamini wa wizara za Serikali.

Alisema lengo la kufanya kikao hicho ni kuwajengea uwezo wa kuweza kujua kizazi chenye usawa, kuratibu na utekelezaji wake kitaifa, hivyo aliwataka kutimiza majukumu yao kwa ufanisi ili kuzidi kuingarisha Tanzania kimataifa.

Aidha alisema kipindi hiki ni maandalizi ya kuandaa Bajeti ya mwaka 2024/2025, hivyo ni muhimu kuijua programu ya usawa wa kijinsia na kuingiza katika sekta zao ili kuweza kutoa ripoti nzuri, zitakazoweza kuisaidia nchi.

Hata hivyo aliwasisitiza kuyaingiza maswala yaliyowekewa ahadi katika sekta husika na kutoa takwimu sahihi na kwa wakati sambamba na kutoa taarifa kwa yaliyofanyika katika sekta zao, ikiwemo sekta ya maji, umeme na kilimo ili taarifa hizo ziweze kuziona na zenye kuridhisha.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto, Siti Abasi Ali aliwataka waratibu wa jinsia kusimamia, kupanga na kuingiza masuala ya kijinsia katika sekta zao ili kutoa wepesi katika utekelezaji.

Hata hivyo aliwataka kuzingatia sheria na kanuni zilizopo nchini ili kuondosha migogoro inayoweza kuepukika.

Mratibu wa programu ya kizazi chenye usawa kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Leah Ipini, alisema programu hiyo itamuwezesha mwanamke kiuchumi na atashiriki katika kazi mbalimbali ikiwemo za kisiasa, kiuchumi na kijamii na kupata kipato cha kuendesha familia na kuepukana na hali tegemezi.

# ZRA yakusanya bil.559.4/- robo tatu ya mwaka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Zanzibar (ZRA), imesema katika kipindi cha Julai mwaka jana hadi Machi mwaka huu imekusanya Sh.bilioni 559.485, kuvuka lengo la ukusanyaji mapato wa Sh. bilioni 536.209.

Kamishna Mkuu wa ZRA, Yusuph Juma Mwenda, aliyasema hayo juzi wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari visiwani hapa.

Kamishna Mwenda alisema hatua hiyo ni ufanisi wa asilimia 104.34, kwamba katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha 2023/2024 makusanyo halisi yaliongezeka kwa asilimia 24.53.

Alisema katika kipindi hicho kiasi cha Sh. bilioni 110.202 zilikusanywa ikilinganishwa ma makusanyo halisi ya mwaka 2022/2023 ambayo yalikuwa ni Sh. bilioni 449.283.

Kamishna Mwenda alisema kwa mara ya kwanza ZRA imefanikiwa kuvunja rekodi ya kuvuka lengo la makusanyo kwa kila mwezi ndani ya miezi tisa ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambayo ni kuanzia Julai hadi Machi.

Aidha alisema kuwa ufanisi huo ukuaji huo unatokana na sababu mbalimbali ikiwemo uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa miundombinu.

Alisema ukuaji pia unatokana na kuimarika kwa huduma za jamii pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zinazotokana na sera nzuri za kiuchumi chini ya Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema kuwa sababu nyingine ni kuimarika kwa shughuli za kiuchumi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, sambamba na kuongezeka kwa uwajibikaji wa ulipaji kodi wa hiyari miongoni mwa walipa kodi.

Mwenda alisema sababu nyingine ni kuongezeka kwa ufanisi wa mamlaka hiyo katika kufanya kazi kwa weledi, kuongeza kwa jitihada za utoaji wa elimu kodi na kuimarika matumizi sahihi ya mifumo ya ukusanyaji kodi ya VFMS na ZIDRAS.

"Kuimarika kwa ushirikiano na taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamisheni ya Utalii, Ofisi za Jeshi la Uhamiaji pamoja na uwepo wa uhusiano mzuri na walipa kodi," alisema Kamishna Mwenda.

Hata hivyo alisema kuwa katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika robo ya nne ya mwaka wa fedha 2023/2024 itakayoanzia Aprili hadi Juni mwaka huu, mamlaka hiyo itaongeza ubunifu kwa kurahisisha na kuondoa usumbufu kwa kuimarisha huduma za kodi kwenye ofisi za kodi za mikoa.

Alisema mkakati mwingine ni kuendeleza weledi wa watumishi wa mamlaka hiyo kwa kuwapatia mafunzo stahiki, usimamizi makini na huduma nzuri kwa walipa kodi pamoja na kuimarisha upatikanaji wa taarifa za wageni wanaoingia Zanzibar.

Alitaja mkakati mwingine ni kuimarisha uhusiano mzuri na walipakodi ikiwemo kusaidia na kurahisisha biashara zao sambamba na kuimarisha matumizi sahihi ya mifumo katika usimamizi wa kodi ikiwemo matumizi ya risiti za kielektroniki na matumizi ya ZIDRAS..



Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Yusuph Mwenda akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, kuhusu hali ya ukasanyaji mapato kutoka Julai 2023 hadi Machi 2024. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama Mjini Magharibi yasikiliza kesi 332 kwa miezi 6

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, amesema kuwa mwenendo wa kesi mahakamani katika Mkoa wa Mjini Magharib Unguja kutoka Oktoba 2023 hadi Machi 2024 kulikuwa na matukio ya uhalifu 332.

Aliyasema hayo mwanzoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari katika makao makuu ya jeshi hilo Mjini Zanzibar.

Kamishna huyo alisema kwa miezi mitatu ya mwisho wa mwaka 2023 kutoka Oktoba hadi Desemba katika mkoa huo wa mjini ambao ndio sura ya Zanzibar kulikuwa na matukio 183 na kwa miezi mitatu ya mwanzo wa mwaka 2024 kutoka Januari hadi Machi kulikuwa na matukio 149.

"Ukiyalinganisha matukuo haya utakuta kwamba kuna upungufu wa matukio 34 lakini twende mbali zaidi ni makosa yapi ambayo yalishamiri katika kipindi hicho ambayo ni udhalilishaji, wizi na shambulio" alisema. Alisema kwa kipindi cha Machi mwaka huu pekee kulikuwa na makosa ya udhalilishaji 14, wizi 26 na makosa ya shambulio nane ambapo katika makosa 14 ya udhalilishaji makosa ya kuingilia kinyume na maumbile saba, kutorosha moja na kubaka sita.

Alisema kwa makosa hayo ya udhalilishaji waathirika ni watoto wa kike mwenye umri kati ya miaka 13 na 17.

Kuhusu makosa ya wizi ambayo ni 26 alisema, uvunjaji kwa kutumia silaha ni manne (4), kuvunja nyumba usiku manne (4) na wizi baada ya kuaminiwa ni makosa 18.

Kamishna huyo alisema makosa hayo sababu zake ni za kimaadili zaidi ikiwemo mmomonyoko wa maadili na masuala ya malezi kwa jamii.

Hata hivyo alisema kwenye hatua za kesi na makosa katika Mahakama ya Vuga, Oktoba 2023 hadi Machi 2024 kulikuwa na kesi 122 ambazo zilipata ushindi mahakamani, washtakiwa 106 waliachiwa huru kutokana na mashahidi kutofika mahakamani kutoa ushahidi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 6948 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**FRANCIS COSMAS**

**By 1: RAMADHANI IDDI KINANGU**
**2: ______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 24th day of April 2024
Dated at 02 this 04 day of 2024

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF BUKOBA, AT BUKOBA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 5260 OF 2024**
**IN THE MATTER OF ESTATES OF THE LATE LAURIAN KAIZA MWAMBARA**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY SWITBERT K. NDEBEA.**

All person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 23rd day of April, 2024.
The will of the said deceased is deposited and open for inspection at the court.
Dated at Bukoba this 28th day March, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE BUKOBA
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **AYUBU MWASEBA MWASIMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye Namba za usajili **T 232 AZK**. Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa katika kituo cha Polisi kilicho karibu nawe. Taarifa Polisi: **PHQ/TAN/TAN/2846/2024.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARCO GODFREY KILONGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1032/0557** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ITIGI SEKONDARI mwaka 2022. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/3453/2024.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GREYSON GODFREY MLOWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 943 AWD. Chassis namba MD2A21BZ3EWB8D320. Engine namba PFZWEB42355. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **MKO/RB/15/2023.**

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai Na. 56/2024**
**JINA LA MDAI ........... MAGUCHI MICROFINANCE COMPANY LIMITED**
**JINA LA MDAIWA ......FRANK LEON MTOLELA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA**
**FRANK LEON MTOLELA**
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba
MADAI YA TSH. 15,885,000/=
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 16 mwezi 04 mwaka 2024 saa 8:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima keleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 Mwezi 03 Mwaka 2024.

HAKIMU

---

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 483/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ADAM MADHEHEBI WA......**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA TULLI ADAM TULLI**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 10 mwezi 05 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 03 mwezi 04 mwaka 2024.

HAKIMU

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**SOSPETER M. MTUKU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2269-0063 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia BUS ANGUMUGU SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **UKE/RB/156/2021.**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 6448 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE;-**
**OTILIA BARNABAS HAULE..............DECEASED**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATIX BY;-**
**LAWRENCE JECKONIA ACKIMU..........PETITIONER**
**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75 of the probate and Administration of Estate rules, CAP 352 R.E 2019)**

ALL person claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 22nd day of April 2024.
Dated at Morogoro this 27th day of March 2024.

Senior Resident Magistrate
Morogoro District Court

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GODFREY ADAMSON MKONDYA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 517 BAD. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MOR/MOR/8397/2024.**

---

## KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI KIWANJA

**MICHAEL HENRICK MLYUKA anatangaza kupotelewa na hati ya kumiliki kiwanja Namba 3395 kilichopo Ruvuma. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Kumbukubu Na. LR/T/2024/3395 RUV.**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 19356 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**

**PIUS JEREMIA MBWILO..............DECEASED**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATOR BY**

**JAMES PIUS MBWILO..........PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75 of the probate and Administration of Estate rules, CAP 352 R.E 2019)**

ALL person claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 30th day of APRIL 2024.
Dated at Morogoro this 28th day of March 2024.

**Senior resident magistrate**
**Morogoro District Court**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 64350 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**GERALD MOZAN MAPEMBE**
**AND**
**In the matter of Application for Letters of Administration by**

- **RASHID AUGUSTINO MAPEMBE**
- **MWANAMISI ZUBERI KEA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**
All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 25th day of April, 2024.
Dated at Korogwe this 26th day of March, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 7068 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**PAUL DAUDI SANGODA**
**AND**
**In the matter of Application for Letters of Administration by LAZARO STEPHANO SANGODA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**
All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 30th day of April, 2024.
Dated at Korogwe this 2nd day of April, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**TANZANIA CHINA TRADE & TOURISM DEVELOPMENT LTD**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI ZENYE NAMBA ZA USAJILI MC 292 DTT, MC 310 DTT, MC 317 DTT na MC 313 DTT. KWA YOYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DAR/ILA/35189/2024.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**TANZANIA CHINA TRADE & TOURISM DEVELOPMENT LTD**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI ZENYE NAMBA ZA USAJILI MC 314 DTT, MC 307 DTT, MC 318 DTT na MC 289 DTT. KWA YOYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DAR/ILA/35189/2024.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**TANZANIA CHINA TRADE & TOURISM DEVELOPMENT LTD**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI ZENYE NAMBA ZA USAJILI MC 636 DNA, MC 177 DJK, MC 190 DJK. KWA YOYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DAR/ILA/35189/2024.**

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Israel yazidi kubanwa kimataifa

**WASHINGTON,** Marekani

LICHA ya Israel kukanusha shambulio lake dhidi ya wafanyakazi wa utoaji misaada katika Ukanda wa Gaza, Marekani imezidi kuibana na kusisitiza tukio hilo ni la kughadhabisha na inahitajika jibu la kutosheleza.

Kauli hiyo imesemwa na Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Lloyd Austin, wakati akizungumza na Waziri wa Ulinzi wa Israel, Yoav Gallant.

Wakati wa mazungumzo hayo yaliyofanyika juzi, Austin alisisitiza umuhimu wa kuchukua hatua madhubti mara moja kwa ajili ya kuwalinda wafanyakazi wa kutoa misaada na raia wa Palestina wanaoishi ukanda wa Gaza.

**Israel ilisema mashambulizi yaliyowaua wafanyakazi hao ililikuwa kosa kubwa na kuahidi kufanya uchunguzi.**

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi ya Marekani, Pat Ryder, alisema kwamba Waziri Austin alimhimiza Gallant afanye uchunguzi wa haraka na wa wazi kuhusu tukio hilo la mauaji ambapo wafanyakazi saba wa shirika la misaada la World Central Kitchen waliuawa siku ya Jumatatu.

Austin alitaka matokeo ya uchunguzi huo yatangazwe hadharani na waliohuska wawajibishwe.

Katika hatua nyingine, majaji watatu wa zamani wa Mahakama ya juu nchini Uingereza, wameungana na wataalam wengine 600 wa kisheria kwa kuitaka serikali yao kukomesha biashara ya silaha kwa nchi ya Israel.

Katika barua waliyomwandikia Waziri Mkuu, Rishi Sunak, walisema uuzaji wa silaha lazima ukomeshwe kutokana na Uingereza iko katika hatari ya kukiuka sheria za kimataifa.

Sunak anakabiliwa na shinikizo kutoka kwa vyama mbalimbali wakitaka kurudi nyuma kuisaidia Israel baada ya wafanyakazi saba wa misaada kuuawa na vikosi vya nchi hiyo.

Mauzo ya silaha ya Uingereza kwenda nchini Israel ni ya chini kuliko mataifa mengine kama Ujerumani na Italia.

Marufuku hiyo kutoka kwa Uingereza itaongeza shinikizo la kidiplomasia na kisiasa kwa Israel, wakati mwenendo wake katika vita ya Gaza unachunguzwa upya kimataifa.

Aliyekuwa rais wa Mahakama ya Juu Lady Hale, ni miongoni mwa mawakili, wasomi na majaji wakuu waliostaafu ambao wametia saini barua hiyo yenye kurasa 17.

Barua hiyo inasema hatua kali inahitajika kuepuka ushiriki wa Uingereza katika ukiukaji wa sheria za kimataifa, ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Mauaji ya Kimbari.

Inaongeza kuwa uuzaji wa silaha na mifumo ya silaha kwa Israel unakiuka majukumu ya serikali chini ya sheria za kimataifa na kuonya juu ya hatari inayowezekana ya mauaji ya kimbari kuwepo Ukanda wa Gaza.

Wakati huo huo, Waziri nchini Israel amekanusha madai kuwa wanajeshi wa Israel waliwaua kwa makusudi wafanyakazi saba wa Shirika la World Central Kitchen (WCK) walipokuwa Ukanda wa Gaza.

Mwanzilishi wa WCK Jose Andres ameishutumu Israel kwa kuwalenga wafanyakazi wake kutoka gari moja hadi lingine.

Hata hivyo, Nir Barkat, ambaye ni mjumbe wa baraza la mawaziri la vita la Israel, aliiambia BBC kwamba kauli ya Andres haina msingi.

Israel ilisema mashambulizi yaliyowaua wafanyakazi hao lilikuwa kosa kubwa na kuahidi kufanya uchunguzi.

Msafara wa misaada ulishambuliwa wakati ukiondoka kwenye ghala la Deir al-Balah, ulikuwa imepakua zaidi ya tani 100 za chakula kwa ajili ya watu wa Gaza.

Msafara huo ulikuwa na magari matatu, yakiwemo mawili yasiyopenya risasi, ambayo yalionyesha wazi nembo ya shirika la hisani. Magari hayo yalikuwa umbali wa kilomita 2.5 na yote matatu yalishambuliwa wakati wa tukio hilo. **BBC**



Mwanajeshi wa Israel akiwa katika ulinzi mkali karibu na majengo machache yaliyosalia ukanda wa Gaza hivi karibuni. **PICHA: REUTERS**

## Spika ajiuzulu kwa kashfa ya rushwa

**PRETORIA,** Afrika Kusini

SPIKA wa Bunge la Afrika Kusini, Nosiviwe Mapisa-Nqakula, ametangaza kujiuzulu baada ya polisi kuvamia nyumba na kufanya upekuzi kutokana na tuhuma ya rushwa inayomuandama.

Mapisa-Nqakula anatuhumiwa kuomba rushwa ili kutoa kandarasi wakati alipokuwa waziri wa ulinzi.

Hata hivyo, amekanusha kuhusika na tuhuma hiyo na kueleza kujiuzulu kwake hakumaanishi kwamba amekubali kuwa ana hatia.



Alisema ameamua kuchukua hatua hiyo kutokana na uzito wa uchunguzi huo na hawezi kuendelea na jukumu lake kwa sasa. Mwanaharakati huyo mkongwe wa mapambano dhidi ya ubaguzi wa rangi aliteuliwa kuwa spika mwaka wa 2021.

Kabla ya hapo, alihudumu kama waziri wa ulinzi kwa miaka saba.

Wiki iliyopita mawakili wa Mapisa-Nqakula waliwasilisha ombi la kutaka amri ya mahakama izuie kukamatwa, wakisema ingemvunjia heshima yake.

Jumanne ya wiki hii, majaji walikataa ombi hilo kwa msingi kwamba suala hilo halikuwa la dharura na hawakuweza kukisia madhara ya kukamatwa wakati bado suala hilo halijafanyika.

Mapisa-Nqakula anashtakiwa kwa madai kadhaa ya kuomba hongo ya kiasi cha Dola 120,000, kutoka kwa mmiliki wa kampuni moja ili kupata zabuni ya kusafirisha vifaa vya jeshi nchini Afrika Kusini kutoka sehemu mbalimbali ya bara la Afrika. **BBC**

## Iran yasisitiza italipiza kisasi



**TEHRAN,** Iran

RAIS wa Iran, Ebrahim Raisi, amesema nchi yake itajibu shambulizi dhidi ya ubalozi wake mdogo nchini Syria, ambalo linashukiwa kufanywa na ndege za Israeli.

Kupitia hotubayake kupitia televisheni, Rais Raisi aliapa kwamba shambulio hilo halitakaliwa kimya na kusisitiza kuwa utawala wake utalipa kisasi dhidi ya watu aliowaita magaidi.

Matamshi hayo ni sawa na yaliyotolewa na kiongozi mkuu wa Iran Ayatollah Ali Khamenei.

Shambulio hilo lililofanyika Jumatatu lililenga sehemu ya ubalozi wa Iran uliopo kwenye mji mkuu wa Syria, Damascus na kuwaua wanajeshi wawili wenye vyeo vya mabrigedia na maofisa wengine wa Kikosi cha Ulinzi wa Mapinduzi cha nchi hiyo.

Awali, Iran ilituhumu Israel kuwa imefanya shambulio hilo na hata Marekani pia inaamini Israel ilihusika na hujuma hiyo. **DW**

# DSTV YAZINDUA MSIMU MPYA WA 'JIYACHIE NA MFALME WA BOMA'

**Na Mwandishi Wetu**

MAMBO yanazidi kupamba moto ndani ya chaneli maarufu ya Maisha Magic Bongo ndani ya DStv ambapo imezindua rasmi tamthilia mpya za Jiya na Dosari kupitia kampeni yake maalum ya Jiyachie na Mfalme wa Boma.

**Uzinduzi huu unathibitisha jitihada za DStv katika kuwapa wateja wake chaguo bora la vipindi na huduma ya televisheni kwa gharama nafuu.**

Msimu huu mpya wa Jiyachie na Mfalme wa Boma umesheheni burudani kadha wa kadha ambazo zinapatikana katika tamthilia na vipindi mbalimbali na msimu huu ukiwa na waigizaji wakongwe na maarufu kama Gabo, Aunty Ezekiel, Mainda, Single Mtambalike, Dk. Almasi, Shamsa Ford, Mary Mtemi na wengineo wengi.

Akizungumza katika hafla ya kuzindua msimu mpya wa Jiyachie na Mfalme wa Boma, Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo amesema kuwa msimu huu mpya umezingatia sana maoni ya watazamaji kuhusu tamthilia za kinyumbani hivyo wanaamini kuwa watazamaji watazifurahia zaidi .

"Wakati wote tunazingatia sana maoni ya watazamaji wetu, ndiyo sababu katika msimu huu mpya wa Jiyachie na Mfalme wa Boma mtashuhudia mabadiliko kadha wa kadha katika vipindi na tamthilia za kinyumbani na yote hii tunafanya ili kuhakikisha kuwa mtazamaji wetu anapata kile anachopenda," alisema Shelukindo.

Aliongeza kusema kuwa moja ya mabadiliko yaaliyofanywa ni pamoja na kuwa na hadithi zinazoakisi maisha halisi ya Watanzania hususani kwenye masuala ya utamaduni na ingizo jipya la waigizaji wakongwe ambao kwa mara ya kwanza wataonekana kupitia DStv.

Pazia la msimu huu mpya wa vipindi vya Maisha Magic Bongo limefunguliwa rasmi na tamthilia ya Jiya iliyoanza kuruka rasmi Jumatatu Aprili 1, 2024.

Tamthilia hii ya kusisimua yenye matukio kadha wa kadha yanayoakisi Maisha ya kila siku katika jamii yetu itakuwa inaruka kila siku ya Jumatano hadi Jumatano saa 1:30 usiku kupitia chaneli ya Maisha Magic Bongo- DStv 160 inayopatikana kwa kiasi cha Sh. 25,000 tu.

Kama haitoshi, kupitia tamthilia ya Dosari, wateja wa DStv wataendelea kupata burudani za kinyumbani zenye drama na matukio ya kusisimua na waigizaji kama Single Mtambalike, Mary Mtemi, Mainda, Dk. Almasi na wengineo wamejipanga kuleta mapinduzi ya burudani na vimbwanga kupitia tamthilia hiyo itakayokuwa inarushwa Maisha Magic Bongo - DStv 160 kila siku ya Jumamosi na Jumapili saa 3:00 usiku.

Shelukindo aliongeza kuwa mbali na msimu mpya wa tamthilia hizo, wateja wa DStv wataendelea kufurahia vipindi vingine mbalimbali ikiwemo ile tamthilia maarufu ya Jua Kali, Huba, Kitimtim n.k

Amewataka wale wote ambao hawajajiunga na DStv kufanya hima kuwahi ofa maalum iliyopo sokoni kwa sasa ambapo mteja hupata seti kamili ya DStv kwa shiling 99,000 tu!

Amesema hii ni ofa ya muda maalum hivyo ni vyema wakaichangamkia ili wasipitwe na moto wa burudani unaoendelea kuwaka ndania ya DStv.



Waigizaji wa tamthilia mpya ya Jiya katika picha ya pamoja wakati wa uzinduzi wa msimu mpya wa Jiachie na Mfalme wa Boma iliyofanyika Aprili 4 2024. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
05.04.2024

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumamosi tarehe 06-04-2024 hadi 08-04-2024 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili:

| | | |
|---|---|---|
| T 203 DYJ / T 837 DJB | T 478 ECF / T 568 EAZ | T 681 DUB / T 572 EAZ |
| T 453 DYG / T 879 EAU | T 684 DUB / T 881 EAU | T 178 DFC / T 777 AQR |
| T 272 EDD / T 394 DVS | T 996 DTN / T 393 DVS | |

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
Urefu - mita 23.00
Upana - mita 4.30
Kimo - mita 5.20

2. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza


## Kundemba na matumaini ya kutoshuka daraja

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kundemba FC imesema ina matumaini makubwa ya kufanya vizuri katika michezo yao 10 iliyobaki katika Ligi kuu ya Zanzibar.

Kundemba ni miongoni mwa timu nne zilizo katika mstari wa hatari wa kushuka daraja kati ya timu 16 za Ligi kuu ya Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya PBZ.

Timu hiyo ipo nafasi ya 13 ikiwa na alama 20 ambapo imeshinda michezo mitano imetoka sare michezo mitano na imefungwa michezo 10 katika michezo 20 waliyocheza katika Ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ali Vuai Shein alisema kutokana na timu ilipo katika msimamo wa Ligi lazima waje na mbinu bora zakiuchezaji ili wafanikiwe kuvuna alama zitakazo inusuru timu isishuke daraja.

Alisema miongoni mwa mbinu hizo ni kutoa hamasa kubwa kwa wachezaji Kwa kila mchezo ili kupambana kwa malengo na kufanikiwa kuvuna alama tatu katika kila mchezo.

"Tuhakikishe wachezaji wanaendelea kuhamasika na kucheza kwa bidii zote ili tupate matokeo yatakayoitoa timu katika nafasi iliyopo na kuipandisha juu," alisema.

## Mashujaa yaikamia Simba Kombe la FA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mashujaa FC, Mohammed Abdallah, 'Bares', amesema licha ya kukiandaa kikosi chake kimbinu, ametumia dakika 180 kuisoma Simba katika michezo ya Kimataifa.

Amesema amewaangalia mchezo wa mkondo wa kwanza na leo atawafuatilia Wekundi hao wa Msimbazi katika mechi ya marudiano ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly nchini Misri.

Hatua hiyo ni baada ya Mashujaa kuwakaribisha Simba uwanja wa Lake Tanganyika , Kigoma katika mchezo wa hatua ya 16 bora ya Kombe la FA Aprili 9, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Bares alisema wamejiandaa vizuri na wanawafahamu Simba lakini amelazimika kutumia mechi mbili za kimataifa kuwaangalia kuona ubora na madhaifu yao kabla ya kukutana nao.

Alisema hatua ya kuwafatilia Simba kwa sababu ya ubora wao na kila mechi wamekuwa na mabadiliko hali inayomlazimu kuangalia kimbinu na kujipanga vilivyo katika mchezo wa hatua ya 16 ya FA.

"Tumekutana na Simba katika ligi hapa nyumbani na walitufunga, wako bora na hii michuano ya Kimataifa inazidi kuwafanya kuwa bora zaidi na kuendelea kujipanga vizuri kwa sababu wanacheza na timu bora Afrika, dhidi ya Al Ahly

## Kocha Geita awajia juu wachezaji

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold, Denis Kitambi, amewashukia wachezaji wake ambao amedai walicheza kwa dharau dhidi ya timu ya Daraja la Pili, Rhino Rangers na kushinda mabao 2-1, juzi kwenye mchezo wa hatua ya 16 bora ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), uliochezwa juzi Uwanja wa Nyankumbu, Geita.

Kitambi alisema katika mechi hiyo ilibidi waondoke uwanjani na mabao mengi, lakini baada ya kupata bao la pili tu, wachezaji wake wakaanza dharau.

Amesema atawaambia wachezaji wake siku nyingine wakiipata timu kama hiyo, inabidi wamalize mechi mapema.

Kocha Mkuu wa Rhino Rangers, yenye maskani yake Tabora amewasifu wachezaji wake kwa kucheza kama alivyowaagiza, lakini tatizo lilikuwa ni viwango vya madaraja.

"Wachezaji walifanya kama nilivyoagiza, ila kwa bahati mbaya tumepoteza mchezo, sababu kubwa ni viwango, wenzetu kidogo wametuzidi daraja, lengo letu lililobaki sasa ni kucheza hatua ya nane bora ya Ligi Daraja la Pili kwa ajili ya kupanda Ligi ya Championship.

Rhino Rangers ni moja ya timu zilizofuzu hatua ya makundi ya ligi hiyo maarufu kama 'first league', ikishika nafasi ya pili kwenye Kundi B ikiwa na pointi 27.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### BRUNO KUUZWA

KLABU ya Newcastle United inahofia huenda wakahitaji kumuuza kiungo wa Brazil Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 26, ili kukidhi sheria za kifedha za Ligi ya England. Miamba wa Ufaransa Paris St-Germain wanaongoza katika mbio hizo, huku Manchester United na Arsenal pia wakimuwania. ***(Sun)***

#### ISAK AWINDWA

TOTTENHAM Hotspur pia wameungana na Arsenal katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 24, iwapo Newcastle United italazimika kuuza wachezaji wake muhimu msimu huu wa joto. ***(Football Insider)***

#### MABEKI WAWINDWA

KLABU ya Newcastle United itapatia kipaumbele usajili wa mabeki wawili wakati dirisha la uhamisho litakapofunguliwa baada ya Mholanzi Sven Botman mwenye umri wa miaka 24 na Jamaal Lascelles mwenye miaka 30, kukabiliwa na majeraha ya muda mrefu. ***(Football Insider)***

#### ATAKIWA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 25, yuko juu kwenye orodha ya washambuliaji wa Arsenal, lakini Sporting Lisbon wanatarajia kipengele cha kuachiliwa kwa mchezaji huyo cha euro milioni 100 kuchochewa ili aondoke. ***(Caught Offside)***

#### KUKATWA MSHAHARA

KIUNGO wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 28, atalazimika kukatwa mshahara mkubwa ikiwa anataka kondoka Manchester City na kurejea Leeds United msimu huu wa joto. ***(Mirror)***

#### BARD ATAKIWA

MANCHESTER United imeanza majadiliano kuhusu kumsajili beki wa Nice mwenye umri wa miaka 23, Melvin Bard. ***(Evening Standard)***

#### KILMAN ATAKIWA MAN

MLINZI wa Wolves, Max Kilman mwenye umri wa miaka 26 yupo kwenye orodha ya wachezaji wanaowania wakati wa uhamisho wa majira ya joto kule Manchester United. ***(Times)***

#### NKETIAH AWINDWA

KLABU ya Leicester City imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Arsenal, Eddie Nketiah mwenye umri wa miaka 24, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Crystal Palace na Brentford. ***(Football Transfers)***

#### FRIMPONG ATAKIWA EPL

ARSENAL, Liverpool na Manchester United ni miongoni mwa klabu za Ligi Kuu ya England zinazomuwania beki wa Bayer Leverkusen, Jeremie Frimpong. Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 23 atapatikana kwa pauni milioni 35 msimu wa joto. ***(Football Insider)***

#### CEBALLOS AVUTIA

KLABU ya Newcastle United inavutiwa na kiungo wa kati wa Real Madrid, Dani Ceballos mwenye umri wa miaka 27. ***(Mundo Deportivo)***

## DONDOO ZA
## MAGAZETI YA



# BARCELONA WAGAWANYIKA KUHUSU MUSTAKABALI XAVI

**Wachezaji wataka kocha mpya mwenye uwezo zaidi, huku Rais na Makamu wake**

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA haijakata tamaa juu ya uwezekano wa kumbakisha Xavi, hata hivyo si wachezaji wote kwenye kikosi hicho wanaamini anafaa kusalia baada ya msimu kumalizika.

**Rais Joan Laporta amebainisha wazi kuwa angependa kuona Xavi anabaki katika klabu hiyo na yuko tayari kumpa kocha huyo raia wa Hispania mkataba mpya.**

Lakini, katika chumba cha kubadilishia nguo, maoni haya hayashirikiwi na wote.

Sport imeripoti kuwa baadhi ya wachezaji wanataka kuona vipaji vipya Camp Nou, kwani wanaamini Xavi amefanya kila awezalo.

Inasemekana baadhi ya wachezaji kikosi hicho wanatamani kuwa na kocha mpya na mwenye uzoefu zaidi. Wachezaji wakongwe, Sergi Roberto na Robert Lewandowski wameelezea masikitiko yao juu ya kuondoka kwake.

Hata hivyo, ripoti za Desemba zilidai kuwa Lewandowski, Ilkay Gundogan, Frenkie de Jong na Marc-Andre ter Stegen hawakufurahishwa kabisa na mtindo wake wa ukocha.

Baada ya maisha marefu kama mchezaji aliyevalia jezi ya Barcelona, Xavi aliajiriwa kama kocha mkuu mwaka wa 2021.

Sasa, inaonekana huenda safari yake inakaribia kuisha, huku akitafuta kuondoka kwa wababe hao wa Katalunya.

Mfarakano unaweza kutokea kwenye chumba cha kubadilishia nguo, lakini watu kwenye chumba cha mikutano hawana nia ya kumuongezea muda Xavi.

Laporta na makamu wa rais Rafa Yuste ndio mashabiki wake wakubwa na wanafahamu kuwa kutafuta mbadala wa Xavi litakuwa swali gumu na wana nia ya kumshawishi kubatilisha kujiuzulu kwake.

# MADRID KUACHANA NA KEPA




**MADRID,** Hispania

REAL Madrid haitarajiwi kumbakisha Kepa Arrizabalaga hadi mwisho wa mkopo wake wa sasa, na hiyo inamaanisha kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 atarejea katika klabu mama ya Chelsea msimu huu wa joto.

Kepa alijiunga na Madrid Agosti kama mbadala wa Thibaut Courtois ambaye aliumia, goti lake la kushoto.

Lakini kupewa nafasi na kocha Carlo Ancelotti, Kepa alijikuta akipoteza nafasi kwa Andriy Lunin tangu Novemba na hajapata nafasi tena.

Huku Courtois akitarajiwa kurejea uwanjani msimu ujao, baada ya kuona kurejea kwake kumecheleweshwa kutokana na jeraha, hivi karibuni Madrid haitamhitaji Kepa tena.

Fabrizio Romano aliripoti kwamba mpango huo huko Bernabeu ni kumwacha Juni na kuongezwa kwa mkataba wa Lunin.

Mkataba wa sasa wa Lunin raia wa Ukraine unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu ujao na 2025 pia ndio wakati mkataba wa Kepa huko Chelsea unamalizika.

Alikuwa namba moja pale Stamford Bridge baada ya kushindana na Edouard Mendy, lakini The Blues wakamleta Robert Sanchez kutoka Brighton & Hove Albion kwa mkataba wa thamani ya pauni milioni 25 na kufungua njia kwa Kepa kuondoka na kutua Madrid, huku huko mwanzo aliripotiwa kutakiwa na Bayern Munich.

Hata kama Sanchez hatachukuliwa kuwa mchezaji wa muda mrefu, Chelsea bado wanahusishwa na Aaron Ramsdale, ambaye anatarajiwa kupatikana baada ya kupoteza nafasi yake Arsenal, na bado wanaweza kumfikiria Djordje Petrovic.

## Mchezaji auawa kwa kupigwa risasi

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

MWANASOKA wa Afrika Kusini, Luke Fleurs ameuawa kwa kupigwa risasi katika utekaji nyara wa gari, timu yake inasema.

Ufyatulianaji huo ulifanyika katika kituo cha mafuta usiku wa kuamkia jana katika kitongoji cha Florida jijini Johannesburg.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alikuwa akisubiri kuhudumiwa alipofikiwa na watu wasiojulikana wenye silaha, ambao walimwamuru ashuke nje ya gari. Mmoja wa washukiwa alikimbia eneo la tukio na gari la Fleurs baada ya kumpiga risasi.

"Washukiwa walimnyooshea bunduki na kumtoa nje ya gari lake, kisha wakampiga risasi moja kwenye sehemu ya juu ya mwili," alisema msemaji wa polisi wa Gauteng, Luteni Kanali Mavela Masondo akiviambia vyombo vya habari. Timu yake, Kaizer Chiefs, imesema kifo hicho kilikuwa "cha kusikitisha".

Ilisema polisi wanashughulikia suala hilo na taarifa zaidi zitawasilishwa kwa wakati unaofaa.

Beki Fleurs alijiunga na Kaiser Chiefs mwaka jana hapo awali aliichezea SuperSport United.

Katika tovuti yake, Kaiser Chiefs imemuelezea Fleurs kama "beki wa kiwango cha juu" na "uwezo mkubwa wa kiufundi".






## Pochettino hajui Nkunku atapona lini

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino ameibua shaka iwapo Christipher Nkunku atachezea klabu hiyo tena msimu huu kutokana na kupona kwake kutokana na jeraha "kuchukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa".

Uhamisho uliosubiriwa kwa muda mrefu wa Nkunku kutoka RB Leipzig ulikamilika msimu uliopita wa joto kwa pauni milioni 52, lakini jeraha la goti katika maandalizi ya msimu mpya lilihitaji upasuaji na Mfaransa huyo hakucheza mechi yake ya kwanza hadi Desemba 19.

Lakini, baada ya mechi kumi, hajaonekana tena tangu fainali ya Kombe la Carabao Februari.

Kwa kuwa msimu umesalia kidogo na Nkunku bado hajarejea mazoezini au hata kukiwa na tarehe inayolengwa ya hilo kutokea, kuna uwezekano mkubwa kwamba hatakuwa tayari kucheza tena hadi 2024/25.

"Sijui. Bado, hatujui," Pochettino alisema wakati akizungumzia hali ya sasa ya utimamu wa mchezaji huyo.

"Kwa sasa hatujui ni lini anaweza kuanza mazoezi na timu, kwa sasa hafanyi mazoezi nasi.

"Kikwazo hakikutokea. Sina taarifa kuhusu hilo. Kupona kwake kunachukua muda mrefu kuliko tulivyotarajia. Hiyo ilikuwa baada ya fainali ya kombe la Carabao.

"Alicheza fainali akiwa na tatizo ambalo hatukujua nalo na kupatikana baada ya mchezo.

"Kuna mazingira tofauti ambayo yanaathiri mambo. Sio yeye pekee. Wachezaji wengi sana wamepata majeraha msimu huu. Tunatumaini anaweza kuhusika tena haraka haraka iwezekanavyo. Itakuwa vizuri sana kama anaweza kujiunga na timu tena kabla ya mwisho wa msimu huu.

## Tembo Warriors kupaa Misri

**Na Saada Akida**

TIMU ya taifa Soka Kwa Watu Wenye Ulemavu 'Tembo Warriors' inatarajia kuondoka nchini Aprili 16 mwaka huu, kwenda Misri katika michuano ya Afrika kwa watu Wenye Ulemavu (AAFCON).

Timu hiyo ipo kambini Arusha kujiandaa na michuano hiyo inayotarajiwa kuanza Aprili 19 hadi 29 mwaka huu na Tanzania imepangwa katika kundi D ikiwa na Angola, Rwanda na Sierra Lione. Wakati Kundi A kuna timu za Cameroon, Misri, Burundi na Nigeria, kundi B kuna Liberia, Morocco, Uganda na Senegal na Kundi C ni Ghana, Kenya, Gambia na Algeria.



Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Shirikisho la soka kwa wa watu Wenye ulemavu Tanzania, TAFF, Vincent Kaduma alisema kikosi kinaondoka mapema kwa lengo la kuzoea hali ya hewa na mazingira.

Alisema wachezaji wanaocheza soka la kulipwa wameungana na wenzao Arusha kujiandaa na michuano hiyo hiyo, wana morali ya kutosha ya kupambana na kupeperusha vyema bendera ya taifa.

"Timu inaendelea na maandalizi yake wapo Arusha kwa ajili ya kambi, kikubwa Watanzania na wadau wa soka kuwaunga mkono wachezaji na kuwaombea dua katika safari yao na kufanya vizuri katika michuano hiyo," alisema Kaduma.

Wakati huo huo Kocha Tembo Warriors, Salvatory Edward (pichani) alisema, mechi za kirafiki wamecheza wakiwa kambini Karatu jijini Arusha zimeimarisha kikosi chake.

# ALLY CHOKI KUIBUKA NA 'KINYAGO' WAKATI WA IDDI

**Na Sabato Kasika**

KIONGOZI wa bendi ya Extra Bongo, Ally Choki, amesema kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani amekitumia kuandaa nyimbo mpya ambazo zitasikika kwa mara ya kwanza wakati wa sikukuu ya Iddi.

Choki ametaja miongoni mwa nyimbo hizo kuwa ni 'Kinyago Changu' ambao amebainisha bila kufafanua kwamba ujumbe wa wimbo huo utawakera wengi hasa wapinzani wa Extra Bongo.

**"Nimeelezea kwa kina kinyago ambacho nimekitengeneza mwenyewe, hivyo ninaelimisha jamii mambo mengi lakini ninaamini wengi watadhani nimewarushia jiwe gizani," alisema Choki.**

Choki alisema ni kawaida baadhi ya watu kujishuku, na kwamba anaamini hilo linaweza kutokea iwapo atakamilisha wimbo huo mpya kutokana na ujumbe uliomo.

Kiongozi huyo aliongeza kwa sasa Extra Bongo inatamba na nyimbo mbalimbali alizotunga mwimbaji huo pamoja na mpya wa 'Penalti ya Mwisho' uliotungwa na yeye Choki.

Extra Bongo iliokufa miaka saba iliopita, ilifufuliwa upya mwaka jana na kuanza kazi Disemba 2 mwaka huo na sasa inaendelea na kazi.

Bendi hiyo imekuwa ikifanya maonyesho mbalimbali ndani na nje ya jijini la Dar es Salaam na sasa imepisha mfungo wa mwezi mtukufu wa Ranadhan ikiwa inatumia nafasi hiyo kujipanga vizuri.

Kwa mujibu wa Choki, Extra Bongo ya sasa inaundwa na wanamuziki wapya, wakiwamo wa zamani wachache, mmojawapo akiwa ni Bob Kissa mwimbaji na Chakuku Tumba (tumba).



Vijana wakiwania mpira wakati walipokuwa walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



# *Siku ya hukumu Simba, Yanga*

INATOKA UKURASA 24

ka zote 90, lakini tumejiandaa kushindana.

"Kupoteza kwenye uwanja wetu wa nyumbani mechi iliyopita ni sehemu ya matokeo na haitufanyi eti tuingie uwanjani tukiwa tumekubali kushindwa, wenzetu walitufunga nyumbani na sisi tunaweza kuwafunga kwao," alisema Chama.

Chama alisema katika mechi iliyopita ilionekana hawakuwa na bahati, huku akimsifu kocha benchika kuwa ni mzoefu hasa anapokuwa kwenye michuano hiyo.

"Tulicheza vizuri uwanja wa nyumbani hatukuwa na bahati tu, tunataka bao la mapema ili kuturudisha kwenye ushindani. Tuna kocha mwenye uzoefu ambaye ametoka kutwaa ubingwa wa Kombe la Shirikisho Afrika ukichanganya na wachezaji wazoefu tuliopo ambao tumepata nafasi ya kucheza hatua ya robo fainali zaidi ya misimu mitatu, kuna kitu kitaongezeka," alisema kiungo huyo raia wa Zambia.

Kwa upande wa Yanga, Kocha Mkuu Miguel Gamondi (pichani) alisema anakiamini kikosi chake kuwa kinaweza kufanya balaa huko Sauzi.

"Kikosi kimefanya vizuri sana kwenye mazoezi, na siku zote mimi ni muumini wa kuamini na kufanya kazi kwa bidii, kupambana na kujituma, nimeona mashabiki wengi wametoka Tanzania na wamekuja kuisapoti timu yao, nawapa hongera sana, hii itatoa chachu kwa wachezaji kupambana kwa bidii mno," alisema Gamondi.

Yanga pamoja na kwamba inahitaji ushindi ili iweze kutinga hatua ya nusu fainali, inahitahi pia sare yoyote ya mabao ili kuweza kuiondosha Mamelodi Sundowns mashindanoni, kwani itabebwa na bao la ugenini, huku yenyewe ikiwa haijaruhusu bao lolote ikicheza nyumbani.

Kanuni za ligi hiyo zinasema hakutokuwa na muda wa nyongeza timu zitakapomaliza kwa sare yoyote ile, badala yake itaangaliwa aliyeshinda bao la ugenini, au mabao mengi ugenini ili kupata mshindi na kama timu zote zitakuwa zimetoka sare zinazofanana nyumbani na ugenini, basi moja kwa moja zitakwenda kupigiania mikwaju ya penalti baada ya dakika 90 za mchezo.

Kanuni hiyo pia inasema hata timu ikishinda idadi ya mabao kama yale ambayo mpinzani wake ameshinda katika mechi ya kwanza, basi moja kwa moja watakwenda kwenye mikwaju ya penalti na si kuongeza dakika.

Kwa maana hiyo, Yanga ilitoka suluhu tena ya bila kufungana na wapinzani wao, na Simba ikashinda bao 1-0 Cairo, basi mikwaju ya penalti itahusika.

# Michezo

Ijumaa Aprili 5, 2024

Nipashe



Barca wagawanyika kuhusu Xavi UKURASA 21




Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya marudiano ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly, kulia ni wachezaji wa Yanga. **PICHA: MTANDAO**

# SIKU YA HUKUMU

## Simba, Yanga kusuka au kunyoa ugenini leo, makocha watamba...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

HATMA ya timu za Tanzania kwenda hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika inatarajiwa kujulikana usiku wa leo, zitakapokuwa ugenini kupeperusha bendera ya nchi katika mechi zao za marudiano hatua ya robo fainali.

Mabingwa wa nchi, Yanga wapo nchini Afrika Kusini, ambapo wao wataanza kushuka kwenye dimba la Loftus Versfeld kucheza dhidi ya Mamelodi Sundowns ya huko, mchezo utaopigwa saa 3:00 usiku wa saa za Tanzania.

**Wawakilishi wengine wa Tanzania, Simba, wataingia uwanjani baadaye, saa 5:00 usiku kwa saa za Kitanzania, kuwavaa Mabingwa Watetezi wa kombe hilo, Al Ahly ya Misri, mchezo ukichezwa Uwanja wa Kimataifa wa Cairo.**

Mechi zote ni za marudiano baada ya zile zilizochezwa Ijumaa na Jumamosi iliyopita Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika mechi iliyochezwa Ijumaa iliyopita, Simba ilipoteza kwa bao 1-0, hivyo ina kazi kubwa ya kulipa kisasi na kuweza kusonga mbele ya michuano hiyo mikubwa barani Afrika.

Ili kusonga mbele, Simba inatakiwa kushinda kuanzia mabao mawili au ushindi mwingine zaidi ya huo, lakini idadi ya mabao iwe inawazidi wenyeji bao moja au zaidi ya hapo.

Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, amesema kila kitu kimekwenda kama kilivyopangwa, na anaamini vijana wake watatekeleza kile ambacho amewaambia uwanja wa mazoezi.

"Kazi yetu kubwa ni kushambulia kwa ajili ya kupata bao la mapema na kuwaweka kwenye presha wapinzani wetu ili wasitushambulie kwa mfululizo.

Nadhani wachezaji wangu wakifanikiwa kupata bao, mechi itakuwa ngumu kwa wenyeji, hatutokaa nyuma, tutashambulia na kuzuia kwa pamoja," alisema Benchika.

Mmoja wa wachezaji waandamizi wa timu hiyo, Clatous Chama alikiri ugumu wa mechi ya leo, lakini watapambana kuhakikisha wanasonga mbele.

"Kazi yetu itakuwa ni kushambulia ili kupata matokeo dakika za mapema licha ya mlima mrefu tulionao, tunategemea mechi itakuwa ngumu kwa daki-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >